BWANA ALILITOA NENO

Somo la Kihistoria ya Maandishi ya Biblia

Malcolm H. Watts

Bwana Alilitoa Neno

Somo la Kihistoria ya Maandishi ya Biblia

Malcolm H. Watts

TBS
Trinitarian Bible Society
William Tyndale House, 29 Deer Park Road
London SW19 3NN, England

Bwana Alilitoa Neno

Product Code: SWHA111
ISBN 978 1 86228 612 2

tbsbibles.org | tbsonlinebible.com
contact@tbsbibles.org

© Trinitarian Bible Society 2025

William Tyndale House, 29 Deer Park Road, London SW19 3NN, England
Registered Charity Number: 233082 (England) SC038379 (Scotland)

Copyright is held by the Incorporated Trinitarian Bible Society Trust
on behalf of the Trinitarian Bible Society.

5M/10/25

Yaliyomo

Agano la Kale 1
Lugha ya kwanza 1
Vifaa vya kuandikia 2
Ufunuo 2
Mafundisho Pacha 3
Lililoandikwa 4
Ya Asili 4
Hekalu 4
Umuhimu wa Sanduku 4
Kitabu Kimoja 5
Nakala 6
Kazi ya Waandishi 6
Kupotea kwa za Asili. 7
Sinagogi Kuu 8
Wamasorete Maarufu 9
Maandishi Ya Wamasorete 10
Muhtasari wa Agano la Kale 10

Agano Jipya. 11
Kweli ya Kikristo Kunakiliwa Chini 12
Asili za Kiungu 12
Kunakili Sahihi. 13
Lahaja katika Maandiko 14
Kuirudisha Andiko Halisi la Agano Jipya 15
Hati za Kiyunani zinazosalia 16
1. *Mafunjo.* 16
2. *Hati za Maandishi ya Herufi Kubwa.* 17
3. *Maandishi ya Herufi Ndogo.* 18
4. *Hadhara.* 19
Uainishaji 19
A. *Maandishi ya aina ya Kibizantini* 20
B. *Aina ya Maandishi ya KiAlexandria* 23
Wakosoaji Washambulia Maandiko ya Kibizantini 25
Toleo Lililoidhinishwa 26
Vidokezo 27

Bwana Alilitoa Neno

Somo la Kihistoria ya Maandishi ya Biblia

Malcolm H. Watts

Biblia ni neno la Mungu la milele. Limetolewa na Mungu kwa mwanadamu ili liwe ndilo mwongozo kamili, kuu, lenye mamlaka, lisilo kosea na lisilo badilika ya Imani na matendo. Katika Makala hii, tutafuatilia historia ya Biblia kutoka mwanzo wake katika ufunuo wa kiungu kupitia udhihirisho wake katika maandishi kwa njia ya uvuvio wa kiungu hadi na upokezi wake kwa usahihi hadi kizazi hiki kwa njia ya uhifadhi kwa majaliwa. Ni Imani yetu ya dhati kuwa, ingawa dhoruba za ukosoaji zaendelea kuvuma dhidi ya Neno la Mungu, Imani ya muumini mnyenyekevu katika Neno lina hakikika na kudhibitika. Juzuu hili takatifu ni – na litadumu kuwa – Kitabu la Mungu.

Agano la Kale

Sehemu kubwa ya Agano la Kale liliandikwa kwa Kiebrania. Ambayo wakati mwingine huitwa "lugha ya Kanaani" (Isaya 19:18) au "lugha ya Kiyahudi" (Isaya 36:11). Labda lilikuzwa kutoka kwa Kiebrania cha zamani kilichosemwa na Ibrahimu kule Uru ya Wakaldayo (Mwanzo 14:13) na baadhi ya wasomi wanaamini kuwa Kiebrania kilimtangulia Ibrahimu nayo ilikwa ndiyo ile "lugha moja" na "usemi mmoja" kabla nyakati za Babeli (Mwanzo 11:1). Yaani, waliamini kuwa ndiyo ilikuwa lugha ya asili ya mwanadamu.

Lugha ya kwanza

Ushahidi wa kudhibitisha mtazamo huu ni mwingi. *Kwanza kabisa*, kwa Kiebrania, majina ya wanyama yaashiria kwa usahihi sana asili na sifa zao – hasa Zaidi, kuliko lugha nyingine yote ya kale. Hili lingelingana na ukweli wa kuwa Adamu punde tu baada ya kuumbwa, aliwapa wanyama majina yao kwa kuangalia sifa zao za kiupekee na asilia za kila aina ya wanyama (Mwanzo 2:19–20). *Pili*, majina sahihi, kama Adamu, Hawa, na Kaini, yana maana msingi katika Kiebrania, ambayo baadhi yao ndiyo yaliyopewa katika Maandiko ya Agano la Kale (Mwanzo

2:23; 3:20; 4:1). *Tatu*, majina ya baadhi ya mataifa ya kale yanaonekana kuwa na asilia ya Kiebrania, yakiwa yametolewa kutoka kwa wana na wajukuu wa Shemu, Hamu na Yafethi: kwa mfano Waasuria kutoka kwa Ashuri; Waelami Kutoka kwa Elamu, na Waaramu kutoka kwa Aramu.

Kwa hiyo, hoja *inaweza* kutolewa kwa ajili ya namna fulani ya Kiebrania kuwa ndiyo lugha ya kwanza kutumiwa na kusikiwa katika dunia hii; lakini hata iwe hivyo, ni ukweli usiopingika kuwa karibu Agano la Kale lote liliandikwa kwa Kiebrania. Isipokuwa sehemu chache zilizo katika lugha ya Kiaramu (lugha inayoelewana kwa karibu na Kiebrania) ambayo pia, kwa hakika, ilichukua mahala pa Kiebrania wakati wa uhamisho. Sehemu hizi ni mbili katika kitabu cha Ezra (4:8–6:18; 7:12–26), ambazo zaelezwa kwa Kiaramu kuwa lugha rasmi ya ufalme wa Uajemi; na aya katika Yeremia (10:11), ambayo ni nukuu ya methali ya Kiaramu; na sehemu kubwa kiasa cha kitabu cha Danieli (2:4 hadi 7:28), ambapo Kiaramu kimetumika labda kwa sababu sehemu hiyo yote inahusiana na mataifa ya dunia.

Vifaa vya kuandikia

Sasa Maandiko ya kale yaliandikwa kwenye nini? Mwanzoni, Maandiko ya Agano la Kale yaonekana kuandikwa kwenye mafunjo. Hayo yalitengenezwa kutoka kwa matete yaliyomea katika kingo za mto Naeli. Matete hayo yalikatwa vipande vipande na kupangwa kwa pembe za kulia moja kando ya nyingine: halafu yalipigwa, shinikizwa na kung'arishwa kutengeneza aina ya karatasi ya kale. Tunajua kuwa matete yalitumiwa Misri hapo zamani, na kwa hakika wakati wa Musa, na kwa hivyo inawezekana kuwa nakala za kwanza za Agano la Kale yaliandikwa katika vifaa hivi. Kama sivyo, basi yangeandikwa katika ngozi ya wanyama ambayo ilitumika hapo mnamo miaka 2,000 Kabla ya Kristo. Ngozi zilikuja kupendelewa kwa sababu zilidumu Zaidi na zilithibitishwa kuwa si nyepesi kuvunjika: kwa hivyo yalihifadhi maandiko kikamilifu zaidi.

Ufunuo

Twajua kuwa Mungu ndiye Mkuu. Maandiko yasema, "Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi?" (Ayubu 11:7). Na jibu litarajiwalo ni, kwa hakika, La. Hatuwezi kwa busara yetu yote kumvumbua Mungu asiye na mwanzo wala mwisho. Yeye yu juu zaidi ya ufahamu wa mwanadamu. Je, hii inamaanisha kuwa hatuna tumaini ya kumjua? Twashukuru kuwa haimaanishi hivyo. Ingawa hatuwezi – hata kwa uchunguzi mkali – kumvumbua Mungu, Yeye aweza kujifunua kwetu. Kama chanzo cha ukweli wote, anaweza kutufundisha kuhusu nafsi yake ya ajabu; na kwa hivyo, kama asemavyo mwandishi wa Zaburi, "Katika nuru yako tutaona nuru" (Zaburi 36:9). Hii inatuleta kwa kawaida kwenye fundisho la ufunuo.

Ufafanuzi mfupi lakini sahihi ya ufunuo inatoka kwa kalamu ya Dkt. James Bannerman aliyesema: "Ufunuo, kama tendo la kiungu, ni uwasilishaji wa ukweli halisi kwa mwanadamu kupitia njia ya kiungu kutoka kwa Mungu. Ufunuo, kama athari ya tendo hilo, ndiyo ukweli halisi unaowasilishwa".[1]

Sasa, ufunuo ni ya aina mbili. Kwanza kabisa, kuna ***ufunuo wa jumla***. Hii huja kwa sehemu, hutoka nje yetu, kutoka kwa dunia inayo tuzunguka. Katika kazi ya uumbaji na utunzaji, Mungu hutuonye-

sha sehemu ya uungu na ukamilifu wake. "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake" (Warumi 1:20; linganisha na (ln.) Zaburi 19:1; Matendo 14:27). Tukiangalia sehemu tofauti ya ulimwengu uonekanao, tunashurutishwa kufikiria kwa hofu yenye heshima, kumhusu mbunifu na muumbaji wa kiungu. Ufunuo wa jumla Zaidi hutoka ndani yetu. Kwa kuwa tumeumbwa kwa mfano wake Mungu, tunayo kiwango cha hisia asili ya Mungu, kutokuharibika, na kutofautisha mema na mabaya. Kama vile Paulo asemavyo, sisi tu sheria kwetu wenyewe kwa sababu "kazi ya torati" iliyoandikwa "mioyoni" mwetu, "dhamiri" yetu ikitushuhudia (Warumi 2:14,15).

Ufunuo wa aina hii ni ya jumla: siyo tu kwa sababu imetolewa kwa ulimwengu kwa jumla, bali pia kwa sababu inahusiana ni vitu vya jumla pekee. Haisemi chochote maalum kama upatanisho na Mungu, msamaha wa dhambi, au njia ya mbinguni.

Hata hivyo, katika rehema zake za ajabu, Mungu amefurahishwa kutupatia ***ufunuo halisi***. Hii pia ina ufunuo wa nje, na wa ndani. Ufunuo Halisi ya nje ulikujua kupitia "Udhihirisho" Mungu akijidhihirisha kwa wanadamu na pia kupitia "sauti" Mungu akiongea nao. "Bwana akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii ..." (Mwanzo 12:7; ln. 3:819). Ufunuo Halisi wa ndani iliwajilia watu teule kupitia maono, ndoto, na mizigo. Kama Mungu mwenyewe alivyosema, "Akiwepo nabii kati yenu, Mimi, Bwana, nitajifunua kwake katika maono, Nitasema naye katika ndoto" (Hesabu 12:6). "Mizigo" zilikuwa jumbe nzito zilizoilemea akili na moyo. Kwa hivyo twasoma, "Mzigo wa neno la BWANA kwa Israeli kumpitia Malaki" (Malaki 1:1). Ufunuo halisi uhudumia mahitaji ya ndani kabisa ya mioyo ya wanadamu. Hujibu swali lililo la zamani kama nafsi ya mwanadamu – "mtu huw mwenye haki mbele za Mungu?" (Ayubu 9:2).

Kupitia Ufunuo wa jumla na halisi (ambao upeo wake ulikuwa, bila shaka, katika kufanyika mwili), Mungu ametupa kwa neema ufunuo wake wa kiungu na ametujulisha njia ya wokovu wake.

Mafundisho Pacha

Kuna mafundisho pacha ambayo sasa tunahitaji kuzingatia: Uvuvio ambayo profesa Louis Gaussen aliwahi kufafanua kuwa ni "ile nguvu isiyoelezeka ambayo Roho wa Mungu aliweka zamani juu ya waandishi wa Maandiko matakatifu, ili kuwaelekeza hata katika kuyachagua maneno waliyoyatumia, na kuwahifadhi sawa kutokana na makosa yote na kuachwa kote".[2]

Uvuvio, basi, ndiyo ile *mchakato* ambayo kupitia hiyo, Mungu hutia ushawishi usio wa kawaida juu ya watu Fulani, akiwawezesha kuandika chochote kilichofunuliwa kwa usahihi na bila makosa. "Watu watakatifu wa Mungu" twasoma kuwa "walinena wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:21). Matukio ya mchakato huu ni Neno la Mungu liliolandikwa, "maandiko ya kweli" (Danieli 10:21). Kauli ya mtume ya kipekee huja akilini mara, "kila andiko limepewa kwa uvuvio wa Mungu" (2 Timotheo 3:16).

Maandiko yaliyovuviwa ni kitabu cha Mungu cha ufunuo. Kama matokeo ya ufunuo na uvuvio, twaweza kushika mkononi Biblia na kujua kuwa tunaimiliki Neno la Mungu lililoandikwa.

Lililoandikwa

Mfano wa kwanza wa nakala ya maandishi aina hii inapatikana katika Kutoka 17:14 ambapo, punde baada ya vita na Waamaleki, Bwana alimwambia Musa "Andika habari hii katika kitabu iwe ukumbusho ..." na pia tena katika Kutoka 24:4, twasoma kuwa "Musa akayaandika maneno yote ya BWANA" na tena pia katika Kutoka 34:27, Bwana alimwambia "Andika maneno haya ..." Na tunaweza endelea hivi. Kuna vifungu vingine vingi yaonyeshayo kuwa Musa aliandika mengi, mengi Zaidi, hata Torati nzima yaani vitabu vitano vya kwanza (k.m. Kumbukumbu 31:9,24–26; Hesabu 33:1,2).

Ya Asili

Yalipoandikwa, ya asili yaliyovuviwa, au "maandishi halisi" (kama yaitwavyo), yalihifadhiwa kwa uangalifu sana.

Musa, kwa mfano, ilikabidhiwa Makuhani walioiweka karibu na Sanduku la Bwana. Twasoma katika Kumbukumbu 31:25,26 kuwa "Musa akawaamuru Walawi waliokuwa wakilichunga sanduku la agano la BWANA akawaambia, Twaeni chuo hiki cha torati [chuo ambacho alikuwa ameiandika] na mkiweke ndani [au kando] ya sanduku la agano la BWANA Mungu wenu ili kiwe kama shahidi juu yako" (ln. Yoshua 1:8; 1 Wafalme 2:3; Nehemia 8:1).

Baada ya Musa, alikuja Yoshua ambaye chuo chake kimetumia jina lake; na kuelekea mwisho wa maisha yake, kulingana na Yoshua 24:26, alifanya kama vile tu Musa alivyofanya awali. Baada ya kuongezea kwa chuo cha Musa, alikichukua chuo hicho na kuibadilisha katika patakatifu. "Na Yoshua akayaandika maneno haya yote katika kitabu cha torati ya Mungu, na akachukua jiwe kubwa na kiweka chini ya mwaloni uliokuwa karibu na hema ya BWANA."

Haikuwa muda mrefu kabla ya kuongewa Zaidi, wakati huu ikiwa ni Samweli aliye "waambia watu madaraka ya ufalme, akayaandika katika kitabu, akaiweka mbele za BWANA" (yaani, mbele za Mungu, katika mahali patakatifu zaidi na kando ya sanduku la agano; 1 Samweli 10:25).

Hekalu

Wakati hema lilibadilishwa na hekalu, haya maandishi halisi yenye thamani yaonekana kuhamishwa katika jengo hilo la kudumu. 2 Wafalme 22:8 pengine yaashiria hayo wakati Kuhani Mkuu Hilkiya amenukuliwa kusema "Nimekiona kitabu cha torati katika nyumba ya Bwana". Baadhi ya wasomi wamependekeza kuwa "kitabu cha torati" kilikuwa maandishi halisi ya Musa, iliyofichwa na makuhani nyakati za enzi za uovu za Manase na Amoni na yaligunduliwa tu wakati huu na mfalme kufahamishwa.[3] Katika Mambo ya Nyakati ya pili 34:14, kimeitwa "kitabu cha torati ya Bwana iliyotolewa kwa mkono wa Musa".

Umuhimu wa Sanduku

Dkt. W. H. Green aonyesha kuwa kuweka nyaraka hizi katika mahali patakatifu ni kwa "mujibu wa matumizi ya mataifa makuu ya zamani". Anadokeza ule ukweli kuwa "Warumi, Wayunani, Wafoinike, Wababuloni na Wamisri walikuwa na maandishi yao matakatifu ambayo yalihifadhiwa kwa wivu katika hekalu zao, na yalikabidhiwa uangalifu wa viongozi walioteuliwa mahususi kwa ajili ya hiyo".[4]

Kando na hiyo, kulikuwa na, sababu za muhimu zaidi kwa nini nakala hizo ziliwekwa mahala pale:

Sanduku liliwekwa katika patakatifu pa Mungu; na maandishi yaliwekwa kando ya sanduku kwa hivyo ilihusishwa kipekee na Mungu. Yeye kwa kweli ndiye mwandishi wa Maandiko. Yale anayoyasema, na yale Maandiko yanasema ni mamoja (Warumi 9:17; Wagalatia 3:2). Hapa, basi, Neno la Mungu lililoandikwa na, haya Maandishi yote yaliyovuviwa, yanaweza kuitwa "maneno ya Mungu" (Warumi 3:2; ln. Matendo 7:38).

Waisraeli watawa walielewa sanduku kuwa ndiyo enzi ya Mungu (Kutoka 25:22; Zaburi 80:1). Ukweli kuwa maandiko haya yaliwekwa kando ya sanduku kuwa yalikuwa yenye *mamlaka ya kimungu*. Maandiko yana mamlaka makuu. Inahitaji kutoka kwa wanadamu, Imani isiyo na shaka katika mafundisho yake na utii usioyumba kwa maagizo yake. Kila nafsi ya mwanadamu lazima kuisujudia. "Maana alikaza ushuhuda katika Yakobo, Na sheria aliiweka katika Israeli. Aliwaamuru baba zetu Wawajulishe wana wao …" (Zaburi 78:5).

Zaidi ya hayo, kwa kuwa maandiko haya yaliwekwa karibu na sanduku, ndani ya hema au hekalu, yalitengwa na vitabu vyote vya kawaida. Yalitangazwa wazi kuwa *takatifu*. Kwa hakika Neno la Mungu lililoandikwa ni safi na tukufu. Ni ukweli usio na mchanganyiko wala kosa lolote. "Maneno ya Bwana ni maneno safi, Ni fedha iliyojaribiwa kalibuni juu ya nchi; Iliyosafishwa mara saba" (Zaburi 12:6). Maandiko yaliyovuviwa yapaswa kuheshimiwa nyakati zote kama "Maandiko matakatifu" (2 Timotheo 3:15).

Sanduku la agano, bila shaka lilikuwa na kiti chake cha rehema ambapo damu ya kafara ilinyunyizwa (Kutoka 25:21); na maandiko yaliwekwa karibu nayo, ikiashiria labda kuwa yalieleza mafundisho ya upatanisho na kuonyesha *njia pekee ya kumkaribia Mungu*. "Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi …" (Luka 24:46,47).

Wazo moja la mwisho: hati hizo zingekuwa chini za mbawa za makerubi (Kutoka 25:18–20), uashirio ya kuwa *zinalindwa na kuhifadhiwa* kimungu. Ingawa hii hupingwa siku hizi, fundisho la kuhifadhiwa kwa Maandiko inapaswa kuaiminiwa na kutangazwa kwa ujasiri. "Agano la Kale katika Kiebrania … na Agano Jipya katika Kiyunani … yakiwa yamevuviwa moja kwa moja na Mungu, na kwa utunzaji wake wa kipekee na uhifadhi imewekwa safi katika vizazi vyote." (Ukiri ya Imani ya Westminster Sura. 1; Sehemu. 8). Bwana wetu mwenyewe alisema: "Mpaka mbingu na nchi itakapoondoa, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie" (Mathayo 5:18; ln. Zaburi 119:152; Isaya 40:8).

Kitabu Kimoja

Mungu aliendelea kuwavuvia watu hadi kukawa na mkusanyiko wa ajabu wa vitabu (1 Mambo ya Nyakati 29:29; 2 Mambo ya Nyakati 9:29, 12:15; Isaya 30:8; Yeremia 36:1,2). Maandishi ya Musa ya kwanza yakadiriwa kuwa mnamo 1450 Kabla ya Kristo (KK), ili hali maandishi ya Malaki yangekamilika mnamo 450 KK. Kwa hivyo ilikuwa takriban miaka 1,000 ambayo Mungu kwa neema yake alizungumza na wanadamu kwa ushawishi wa kiungu wa

Roho Mtakatifu, akasababisha maneno yake yaandikwe chini, yakiwa huru kutoka kwa makosa yote katika ukweli wa mambo na katika mafundisho. Maandishi haya basi yakahifadhiwa kwa njia ya ajabu. Kilichobakia kwetu ni kuzingatia hapa kuwa, kuanzia mwanzo wake, mkusanyiko huu ulikubalika kama kitabu kimoja iliyoitwa "Kitabu chake BWANA" (Isaya 34:16).

Nakala

Mara ya Kwanza kunakili inatajwa ni kuhusiana na Amri Kumi, zilizoandikwa mwanzoni bila shaka katika mbao za mawe kwa kidole cha Mungu. Zile mbao za kwanza zikisha vunjika, Bwana alimwagiza Musa kuchonga mbao mpya na Bwana akayaandika maneno yale yale. Ilikuwa ni hapo ndipo Mungu aliweka chini mwongozo wa kunakili: nakili lazima iwe "chapa wa maandiko ya kwanza" (Kumbukumbu 10:4). Na tuna misingi imara kuamini kuwa mwongozo huu ulitekelezwa madhubuti. Wakati ujumbe wa Yeremia ulipoharibiwa na mfalme Yehoyakimu, Mungu alimwambia nabii huyo atengeneze nakili nyingine, lakini katika kutenda hivyo, alibainisha kuwa sharti iwe nakala halisi. "Haya! Twaa wewe gombo lingine, ukayaandike ndani yake maneno yote ya kwanza, yaliyokuwa katika gombo la kwanza, ambalo Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, ameliteketeza" (Yeremia 36:28). Ipasavyo, Baruku (mwandishi wa Yeremia) aliandika upya, chini ya agizo la nabii, maneno yote yaliyokuwa katika hati ya awali (36:32 – kwa hivyo, gombo la pili lilikuwa nakala halisi ya la kwanza, ingawa kwa wakati huu Baruku aliongezea maneno mengine kutoka kwa huduma ya Yeremia iliyovuviwa).

Kwa hivyo nakala zilitolewa siyo tu ya Amri Kumi, bali pia za sehemu zingine za Maandiko. Nakala ya kitabu cha Kumbukumbu, au labda ya vitabu vya Musa vitano vyote, vilipaswa kuwa katika mikono ya kila mfalme wa Israeli. "Tena na iwe, zamani aketipo juu ya kiti cha ufalme wake, ajiandikie nakala ya torati hii katika chuo, kufuata hicho kilicho mbele ya makuhani Walawi" (Kumbukumbu 17:18; ln. 2 Mambo ya Nyakati 23:11). Bila shaka, za asili zilikuwa mikononi mwa "makuhani na Walawi" na inaposema, "ajiandikie nakala", pengine hii haimaanishi kuwa yeye mwenyewe ajifanyie hivyo bali kuwa apange mtu kumfanyia hilo (ln. 1 Samweli 1:3; 13:9; 1 Wafalme 8:62; Yohana 19:19, ambapo watu wengine wanasemwa kuyafanya yale, ambayo katika matukio kwa hakika yalifanywa na wengine).

Ilikuweza kuhudumu vema, Waamuzi wangehitaji kuwa na sehemu tofauti za torati ya Musa (2 Mambo ya Nyakati 19:10), kama vile makuhani pia, na zaidi wale waliotumwa na Walawi kufundisha katika miji ya Yuda (2 Mambo ya Nyakati 17:7–9). Katika tukio la mwisho, imewekwa haswa kuwa "Wakafundisha katika Yuda, wenye kitabu cha torati ya Bwana" (v 9). Hatupaswi kudhania kuwa ni viongozi pekee ndio waliokuwa na nakala za Maandiko. Kuna ushahidi wa kupendekeza kwamba walioamini kwa jumla waliweza kupata vitabu vya Biblia (Zaburi 1:4, Zaburi 119).

Kazi ya Waandishi

Maandishi halisi, kama tulivyoona, yanatambuliwa "ya asili". Nakala yanatambuliwa "ya nakili". Ni wazi kuwa umakini mkubwa ulichukuliwa katika kunakili Maandiko. Mwanzoni, makuhani walijukumika katika hili (Kumbukumbu 17:18) lakini baadaye waandishi (katika

Kiebrania: *sopherim*, kutoka *saphar*, ku andika) walichukua jukumu hilo, kama vile lugha ya nabii Yeremia yaonyesha: "Mnasemaje, ... torati ya Bwana tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo" (Yeremia 8:8). Wale ambao mwanzoni walitengwa kuwa waandishi walikuwa na majukumu mengi na tofauti. Lakini, jinsi muda ulivyopita ndivyo walivyozingatia kazi ya kunakili: na hivyo mtu kama Ezra alikuja kuitwa "mwandishi wa maneno ya amri za Bwana, na wa sheria zake alizowapa Israeli" (Ezra 7:11).

Inaeleweka kwamba, uhitaji wa nakala za Maandiko ukawa mkubwa sana. Kwa hiyo waandishi walijigawa wenyewe kutengeneza "familia" au "makundi", wakiunganisha juhudi zao ili kuhakikisha matokeo bora zaidi (1 Mambo ya Nyakati 2:55). Ustadi wao katika nyanja hii, pamoja na staha yao kuu kwa Maandiko Matakatifu, ilimaanisha kutokeza nakala bora kabisa. Kwa kweli, ni hati-kunjo tu zilizotoka katika kundi hili la waandishi ndizo zilizotegemewa.

Inastahili kuzingatiwa hapa tu kwamba, katika madhumuni na uongozi wa Mungu, Wayahudi walitunza sana maandishi yao matakatifu kuliko watu wengine wowote katika ulimwengu wa kale.

Usahihi wa aina hiyo ulipatikana kiasi cha nakala za waandishi zingeweza kutajwa kuwa Neno halisi la Mungu na kwa hiyo lenye mamlaka ya kimungu. Katika 1 Wafalme 2:3, Daudi amwamuru Sulemani, mwanawe: "uyashike mausia ya Bwana, Mungu wako, uende katika njia zake, uzishike sheria zake, na amri zake, na hukumu zake, na shuhuda zake, sawasawa na ilivyoandikwa katika torati ya Musa". Sasa Mfalme Sulemani angeweza tu kupata nakala, kama inavyotajwa katika Kumbukumbu la Torati 17:18,19; lakini angalia jinsi nakala hii inavyofafanuliwa kama "iliyoandikwa katika torati ya Musa". Uangalifu huo wenye bidii uliongoza kazi ya kunakili hivi kwamba hati iliyotokezwa ilidumisha mamlaka ya maandishi ya asili. Lilikuwa Neno la Mungu na lingeweza kutajwa hivyo.

Kupotea kwa za Asili

Yerusalemu iliwaangukia Wababeli mwaka wa 586 KK. Mji ulipata uharibifu mkuu na hekalu kuu lililojengwa na Sulemani liliharibiwa kabisa (2 Mambo ya Nyakati 36:17–19). Ingawa haikutajwa katika historia, ni karibu hakika kwamba maandishi ya asili yaliangamia pamoja na jiji hilo. Walakini, yote hayakupotea. Kufikia wakati huo nakala nyingi zilikuwa zimefanywa na baadhi ya hizi zilichukuliwa hadi katika nchi ya utumwa; kwa maana twapata Danieli akinukuu kutoka katika kile ambacho lazima kilikuwa nakala ya Sheria ya Musa (Danieli 9:11) na pia akitaja unabii wa Yeremia, ambao lazima nakala yake iwe pia miliki yake (9:2).

Mnamo 537 KK, Wayahudi walianza kurudi kutoka utumwani na twajua kwamba Ezra alianzisha tena ibada huko Yerusalemu "kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Musa" (Ezra 6:18). Hilo ladokeza kwamba bado walikuwa na nakala za Maandiko na kwamba waliweza kuzichunguza walipopanga ibada kwa ajili ya hekalu la pili. Kulingana na Nehemia 8:1, watu walimwomba Ezra ailete "kitabu cha torati ya Musa, ambayo BWANA aliwaamuru Israeli" Hii haikuwa nakala halisi – bali ilikuwa nakala tu – lakini kwa umuhimu inaelezewa kwa "sheria ya Musa". Tunahitimisha kutoka kwa Maandiko hayo kwamba Mungu alikuwa amehifadhi Neno Lake kwa njia ya ajabu.

Sinagogi Kuu

Historia ya Agano la Kale inaisha ghafla kwa kurudi kutoka uhamishoni; lakini, kulingana na vitabu vya baadaye, Ezra anaonekana kutwaa uongozi juu ya kikundi cha watu wenye elimu na hekima (Nehemia 8:4,7,13; taz. Ezra 7:6,11,22). Mapokeo ya Kiyahudi yanatufahamisha kwamba, baada ya Wayahudi kurudi, Ezra aliianzisha Sinagogi Kuu kwa nia ya kupanga upya maisha ya kidini ya taifa. Baraza hili – kwa maana ndivyo lilivyokuwa – lilikuwa na washiriki 120 na likaja kujumuisha nabii Hagai, Zakaria na Malaki. "Wanaume wa Sinagogi Kuu" walikusanya pamoja nakala zote za Maandiko Matakatifu ambazo wangeweza kupata. Haya, waliyafanyia uchunguzi wa kina na kulinganisha. Makosa mengi madogo, yaliyofanywa bila kukusudia, sasa yalisahihishwa. Makosa haya yalikuwa kama vile kuachwa kwa herufi, neno, au pengine hata mstari. Kwamba zilikuwa zimejipenyeza katika hati fulani haishangazi hata kidogo tunapokumbuka kwamba kuna angalau jozi nane za herufi za Kiebrania zinazofanana, hata kufikia hatua ya kuwa karibu kuwa sawa. Waandishi waangalifu zaidi hawakuwa juu ya kufanya kosa dogo. Hatimaye, hata hivyo, nakala hizo zilifanyiwa marekebisho na ikiwa yoyote ilipatikana kuwa makosa maalum, ilizikwa katika "genizah", mahali patakatifu karibu na sinagogi la Kiyahudi. Kama matokeo ya kazi ya Sinagogi Kuu, Hekalu la Pili inaonekana kuwa lilitolewa na maandishi yanayofanana sana na maandishi ya Kiebrania yaliyopokelewa baadaye.[5]

Kufikia wakati wa Bwana wetu dunaini, nakala nyingi zenye kutegemeka zilipatikana. Bwana Yesu mara kwa mara alikata rufaa kwa Maandiko matakatifu. Alisoma kutoka kwayo katika masinagogi (Luka 4:16); Alinukuu kutoka kwayo katika huduma yake ya hadharani (Mathayo 19:3–5; 21:16,42); na aliwahimiza wasikilizaji wake wajisomee wenyewe (Yohana 5:39). Hakuwezi kuwa na shaka kwamba alizichukua nakala zilizokuwepo kuwa Neno la Mungu. Ijapokuwa Alisahihisha fasiri na maandishi ya Kifarisayo, hata siku moja Hakutilia shaka uadilifu wa maandishi ya Kiebrania. Aliweza kusema, "Imeandikwa" (Mathayo 4:4,7,10) na, tena, "Maandiko hayawezi kuvunjwa" (Yohana 10:35). Hiyo inatumika, bila shaka, kwa Mitume (Matendo 1:16, 4:25, 28:25; Waebrania 1:1,6,7; nk).

Inaweza kusemwa kuwa hii inathibitisha mengi sana, kwa kadiri ya Septuagint (LXX: tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale iliyofanywa na Wayahudi wa Aleksandria karibu 250 KK) pia inanukuliwa mara kwa mara katika Agano Jipya, bila hata mara moja kutiliwa shaka. Kwa hiyo, kwa msingi huohuo, je, hiyo haingeweza kusemwa kuonyesha kwamba Septuagint ni maandishi yaliyopuliziwa na sahihi? Hapana, kuna kasoro kubwa katika mawazo kama hayo. Ukweli ni kwamba kuna sehemu kadhaa katika Agano Jipya ambapo toleo la Septuagint linaonekana kukataliwa kimakusudi (k.m., Mathayo 2:15, ambapo LXX inasomeka: "Kutoka Misri naliwaita watoto wake"; Warumi 10:15, ambapo LXX inasoma, "Mimi nipo kama majira ya uzuri juu ya milima, kama miguu yake mtu anayehubiri habari njema ya amani." Ona pia: Warumi 11:4; 1 Petro 4:8).

Ingawa baadhi ya manukuu ya Agano Jipya yanaonyesha upendeleo kwa tafsiri ya Septuagint, tofauti katika kesi hizi

zitaonekana kuwa ndogo sana, na sio maana kabisa (k.m., Mathayo 15:8,9 – Kiebrania: "… mioyo yao wameiondoa mbali nami, na kunicha kwao kumekuwa amri ya wanadamu, jambo la fundisho"; Matendo 13:34 – Kiebrania: "Nitakupa rehema za hakika za Daudi", lakini andiko la Kiyunani la Agano Jipya kwa hakika linanukuu. Septuagint hapa, kama vile kwenye ukingo wa Tafsiri yetu Iliyoidhinishwa: "[Nitawapa] … mambo matakatifu ya Daudi, mambo ya hakika").

Zaidi ya hayo, kusudi la kunukuu Tafsiri ya Septuagint mara nyingi ni kuleta kwa uwazi zaidi kile kilichokusudiwa asili (Taz: Warumi 10:18, ambapo tafsiri ya "sauti" inapendekezwa zaidi kuliko ile ya Kiebrania "mstari", usemi usioeleweka kwa kiasi fulani, ingawa kama "kamba" ya ala ya muziki, ina maana kubwa sana. kitu sawa).

"Hatuoni", asema Dkt. Roger Nicole, "mfano wowote wa utambuzi au matumizi kwa Agano Jipya ya ufahamu wa kimantiki kutoka kwa Septuagint na ambayo hayawezi kudumishwa kwa msingi wa maandishi ya Kiebrania". Anamalizia hivi: "Utumizi wa LXX katika kunukuu hauonyeshi kwamba waandishi wa Agano Jipya wamefikiri kwamba toleo hili lilivuviwa yenyewe … Lakini utayari wao wa kutumia LXX, ijapokuwa na kasoro za hapa na pale, unafundisha somo muhimu, kwamba ujumbe wa msingi ambao Mungu alikusudia kuutoa unaweza kuwasilishwa hata kwa njia ya tafsiri, na rufaa inaweza kutolewa kwa toleo kwa kadiri inavyokubaliana na ya asilia".[6] Tukirudi kwa ile hoja yetu ya awali: uthibitisho uliotolewa na Bwana wetu na mitume wake kwa maandishi ya Kiebrania yaonyesha kuwa maandishi hayo kuwa ni sahihi na ya kutegemeka pia.

Wamasorete Maarufu

Kama tulivyoona, Mungu aliinua waandishi, au sopherim, kutoa maandishi safi kabisa. Iliwaangukia wengine kuendeleza kazi yao na kuchukua hatua zinazohitajika kwa uhifadhi wa maandishi. Hawa walikuwa Wamasorete, jina linalotokana na neno la Kiebrania "Massorah" ambalo linamaanisha "mapokezo". Walikuwa familia za wasomi wa Kiyahudi na wachambuzi wa maandishi ambao hatimaye walifungua shule, moja huko Tiberio (kwenye pwani ya bahari ya Galilaya) na nyingine huko Babeli (Mashariki). Hakuna ajuaye ni lini haswa Masorete kwanza alionekana. Wengine wanaamini kuwa wanaweza kufuatiliwa hadi karne ya kwanza BK. Wengine huweka tarehe ya mwanzo wao baadaye, mahali fulani karibu 500 BK. Ipi ni sahihi, mafanikio ya Wamasorete ndiyo ya maana sana.

Yerusalemu ilikuwa imeharibiwa mwaka wa 70 BK. Kwa sababu hiyo, Wayahudi walitawanyika katika nchi mbalimbali za Milki ya Roma. Wamasorete walijua kwamba Wayahudi hao waliotawanywa na vizazi vilivyofuata wangehitaji nakala za Maandiko Matakatifu na waliamini kwamba mambo fulani yangeweza kufanywa ili kuhakikisha kwamba maandishi safi ya Kiebrania yamehifadhiwa. Kwa kuzingatia hili, walikusanya habari muhimu kuhusu maandishi na kuweka sheria za kina za kunakili ifaayo.

Walianzisha alama za vokali (Kiebrania hakina vokali), lafudhi zisizobadilika (ili kuhakikisha matamshi sahihi), walifafanua maana ya maneno (ambapo utata ulikuwepo), walitoa usomaji wa pambizoni (kuondoa upofu), na kuweka alama za kutua zilizokusudiwa (ambazo mara nyingi

huathiri maana). Walikuwa waangalifu sana katika masomo yao hata walihesabu aya, maneno, na herufi za Agano la Kale, wakibainisha kwa mfano, kwamba Alefu hutokea mara 42,377; Beth, mara 38,218; Gilli, mara 29,537; Na kadhalika.

Wanakili walipaswa kufuata sheria kali za Talmud, ambazo zilihusisha yafuatayo: ngozi za wanyama safi pekee ndizo zilipaswa kutumika; kila ngozi lazima iwe na idadi sawa ya nguzo; ilipaswa kuwa na si chini ya mistari arobaini na nane na si zaidi ya sitini; wino mweusi ulipaswa kutayarishwa kulingana na maandalizi fulani; hakuna neno au herufi ambayo ingeandikwa kutoka kwa kumbukumbu; ikiwa hata herufi iliachwa, au kuingizwa kimakosa, au hata ikiwa herufi moja iligusa nyingine, karatasi hiyo ilipaswa kuharibiwa; makosa matatu kwenye ukurasa yalimaanisha kuwa hati nzima ilihukumiwa; na marekebisho ya nakala ilibidi yafanyike ndani ya siku 30, kwa maana vinginevyo ilibidi kukataliwa. Nakala iliyonusurika katika mchakato huu haiwezi kuwa chochote ila sahihi ajabu.

Maandishi Ya Wamasorete

Kusudi la Wamasorete ilikuwa kuhifadhi Agano la Kale kutokana na kila aina ya badiliko; na ili kutimiza lengo hilo ndipo wakafanya mkusanyo wao wa maelezo ya kina (Massorah). Wayahudi waliita kazi yao iliyomalizika "Uzio wa Sheria". Kama matokeo ya juhudi zao, leo tunayo maandishi yaliyo alama ya kawaida na ya jadi.

Maandishi ambayo Toleo letu lililoidhinishwa lilitafsiriwa linaitwa Andiko la Ben Chayyim (baada ya Jacob ben Chayyim, ambaye chini ya uhariri wake lilichapishwa mnamo 1524–5) na linafanana na Andiko la Ben Asher (aliyeishi karne ya kumi huko. Tiberio, huko Palestina, na ambaye, pamoja na washiriki wa familia yake, walianzisha toleo sahihi la Maandishi ya Wamasorete). Hili ni andiko la uaminifu na linalotegemewa.

Kupitia utunzaji wa pekee wa Mungu, tunaweza kusema kwa uhakika kwamba katika maandishi ya Kiebrania ya Kimasorete tuna maandishi ambayo yanakaribiana sana na Maandishi ya Awali ya Kiebrania.

Muhtasari wa Agano la Kale

Kwa muhtasari, basi, ni njia zipi ambazo Mungu alitumia ili kuhakikisha kwamba Neno Lake limehifadhiwa?

La kwanza lilikuwa heshima kubwa ya Wayahudi kwa Maandiko Matakatifu. Myahudi angetetemeka kihalisi mbele ya Neno lililoandikwa. Kulingana na Philo na Yosefo, wangeafadhalisha mateso yoyote, na hata kifo chenyewe, badala ya kubadili chochote katika Maandiko Matakatifu. Mungu alitumia heshima hii kwa andiko ili kulizuia lisipotoshwe na kupotoshwa.

Pili, kulikuwa na amri kuu za Maandiko, kama vile Kumbukumbu la Torati 4:2: "Msiliongeze neno niwaamurulo, wala msilipunguze". Amri hizi, zilizotolewa na mamlaka ya kimungu, zilitia woga wa kweli katika mioyo ya wanadamu.

Tatu, hati-kunjo hizi ziliwekwa katika Patakatifu pa Patakatifu. Kulikuwa hakuna mahali takatifu zaidi duniani, iliwaweka nje ya kufikiwa na mikono inayoingilia.

Nne, weledi mtupu ya waandishi na Wamasorete ililinda na kuhifadhi maandishi safi. Walikuwa wasomi wakubwa,

wenye ujuzi katika sheria ya kimungu na kuheshimiwa kama wafasiri wa Maandiko Matakatifu.

Tano, kulikuwa na uangalizi wa manabii. Katika kipindi chote cha Agano la Kale, manabii walifanya huduma ya kipekee na waliweza kusimamia kazi ya kunakili. Hitilafu yoyote katika unukuzi ingegunduliwa nao haraka.

Sita, Wayahudi walikariri mara kwa mara Maandiko yao, kama vile Kumbukumbu la Torati 6:7 lionyeshavyo wazi: "Wafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo chini, na uinukapo". Marudio haya yaliunda ujuzi wa maandishi hivi kwamba kama neno lingebadilishwa, ingegunduliwa mara moja na, bila shaka, upinzani mkali na hata ukali ungefanywa.

Saba, Kristo na mitume wake walithibitisha Maandiko kama yalivyopokelewa katika nyakati zao. Maandishi ya kawaida yanayotumiwa nao ni sawa na tunayoyatumia leo. Kunukuu kwao bila kusita kuwa Neno la Mungu ni muhuri usiopingika wa uhalisi na kutegemeka kwalo.

Mawazo haya na mengine yanatufanya tuamini kwamba Mungu amehifadhi kwa njia ya ajabu maandishi ya Agano la Kale. Wakati Agano la Kale linasomwa, kulingana na maandishi ya Kimasorete, tunaweza kuamini kwamba tunasoma na kusikia Neno la Mungu. Ingawa zinaweza kupendeza, haituhusu sisi kukubali tafsiri za pekee kutoka kwa Gombo za Bahari ya Chumvi, kutoka katika toleo la Kilatini, au kutoka kwa chanzo kingine chochote.

Mungu *amelihifadhi* Neno lake. Hili halipaswi kueleweka kuwa lina maana kwamba, katika historia yote, Mungu Amefanya miujiza ya kurudiwa-rudiwa, wala kwamba "Aliwavuvia" waalimu na waandishi mbalimbali waliofanya kazi kwenye maandishi. Tunakubali kwamba maandishi ya halisi zimepotea kitambo na kwamba baadhi ya hitilafu zimeingia kwenye nakala zinazopatikana kwetu. Kwa hivyo kuna haja ya uchambuzi wa maandishi. Fundisho la "uhifadhi kwa utunzaji" linahitaji ufafanuzi makini. Je, tunamaanisha nini hasa? Hapa, ningenukuu maneno ya Profesa John H. Skilton: "Mungu ambaye alitoa Maandiko, ambaye hufanya mambo yote kulingana na shauri la mapenzi yake, amelitunza sana Neno lake, amelihifadhi katika vizazi vyote katika hali ya usafi muhimu, na ameiwezesha kutimiza kusudi alililoitoa".[7]

Maandishi ya Kiebrania, basi, yalitolewa awali na Musa na manabii; ilinakiliwa kwa uaminifu na waandishi, iliyosawazishwa na Ezra pamoja na Watu wa Sinagogi Kuu, iliyoidhinishwa na Bwana wetu na mitume Wake, na kuhaririwa kwa uangalifu wa kina na Wamasorete. Uhalisi inahitaji kwamba tuthibitishe kwa ujasiri imani yetu katika Agano la Kale kama ilivyotafsiriwa kutoka kwa maandishi ya Kiebrania ya Kimasorete.

Agano Jipya

Bwana Yesu Kristo alitoa mamlaka iliyovuviwa kwa Maandiko ya Agano la Kale (Mathayo 5:18; 15:3; Marko 12:36; Yohana 10:35). Pia aliahidi kwamba, baada ya kurudi kwake mbinguni, angemtuma Roho wa Mungu ili kuwasilisha ukweli zaidi kwa watumishi Wake wateule na kuwawezesha kuuandika. Hili lingeipatia Kanisa la Kikristo mwongozo usio na dosari. "Msaidizi", *Alisema*, "Roho Mtakatifu,

ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:14, 26; taz.16:12,13).

Mwanzoni, kulikuwa na mafundisho ya mdomo tu. Upesi ikawa wazi kwamba kweli ya Kikristo ilihitaji kuandikwa. Jambo moja ni kwamba mitume (mashahidi wa Bwana wetu katika siku za mwili Wake) walikuwa wanaanza kusafiri kwenda nchi za mbali na muda si muda wote wangeondolewa na kifo (2 Timotheo 4:6; 2 Petro 1:14); kwa mwingine, idadi inayoongezeka ya waongofu wapya na makanisa walikuwa wakihitaji maelekezo ya mara kwa mara, ya kina, na ya kina (Luka 1:3,4; Matendo 1:1); na kwa maana maandishi mengine ya uwongo na uzushi, ambayo hata wakati huo yalikuwa yanasambazwa, yalikuwa yanaleta mkanganyiko mkubwa wa mafundisho (2 Wathesalonike 2:1,2; 3:17).

Roho Mtakatifu, akitarajia haya yote, aliweka mvuto Wake usio wa kawaida kwa watu fulani waliochaguliwa ili waandike kile ambacho kilikuwa kisichoweza kukosea na kisicho na makosa. Kwa hiyo, mwishoni mwa Injili yake, Yohana anajieleza kuwa "mwanafunzi ashuhudiaye mambo haya, na kuyaandika haya", na kuongeza, "tunajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli" (Yohana 21:24,25; taz. 1 Wakorintho 14:37; Wagalatia 1:20; Wafilipi 3:1; 1 Yohana 1:4; n.k.).

Kweli ya Kikristo Kunakiliwa Chini

Hivyo Maandiko ya Agano Jipya yalitokea. Mwanzoni, ziliandikwa kwa Kiyunani ambayo ilikuwa lugha ya kawaida ya Milki ya Roma wakati Ukristo ulipoanza. Uandishi huo ulifanywa kwa nyenzo zilizotayarishwa maalum: "papyrus" (kitu kama karatasi, kilichotengenezwa kutoka kwa shina la mmea wa mafunjo) na, baadaye, "ngozi" (ngozi ya mnyama, inayoitwa "vellum" ikiwa ni nzuri sana kwa ubora). Katika umbo la nje, hati zingeonekana kama hati-kunjo (kama mafunjo) na vitabu (ikiwa ni ngozi au vellum). Jina la kiufundi la hiyo ya mwisho ni kodi (umoja ambao ni kodeksi).

Kuhusu kalamu zilizotumika, zingekuwa za mwanzi au kalamu (zilizotengenezwa kwa mabua au manyoya) na wino karibu bila shaka ungekuwa mweusi na wa kaboni (uliotayarishwa na masizi na kuchanganywa na sandarusi). Baadaye, katika karne ya tano hivi, wino mwekundu wa metali (uliotayarishwa kutoka kwa tufaha-nyongo) ulitumiwa, lakini hii inaonekana tu ilitumiwa kukazia.

Kuna, bila shaka, marejeo katika Agano Jipya ya "kuandika", "karatasi na wino", na pia "vitabu" na "parchments" (yaani ngozi zilizoandaliwa). Tazama: 2 Timotheo 4:13; 2 Wakorintho 3:3; 2 Yohana 12; na 3 Yohana 13. Swali la kuvutia sasa linatokea: Ni nini kilifanyika kwa hati hizi za asili?

Asili za Kiungu

Maandiko hayo yalitambuliwa mara moja na Wakristo wa mapema kuwa yenye mamlaka ya kimungu (1 Wakorintho 14:37), maandiko haya yalisomwa kwanza na wale waliotumiwa, wawe watu binafsi au makanisa, na kisha yakasambazwa ili wengi iwezekanavyo waweze kufaidika na mafundisho ya mitume (1 Wathesalonike 5:27; Ufunuo 1:3; Wakolosai 4:16; 2 Petro 3:15,16). Cha kusikitisha ni kwamba, nakala hizi asili (au "autographs") hazingeweza kudumu kwa muda mrefu, kwa

kiasi fulani kwa sababu zilikuwa tete na matumizi ya mara kwa mara yalizisababisha kusambaratika, na kwa sababu, kwa sehemu, yalikabiliwa na hatari za ajali pamoja na mateso.

Kunaweza kuwa na marejeo ya maandishi asilia katika risala ya mwaka wa 200 BK. Tertullian, mmoja wa Mababa wa Kanisa la Mapema, aliwajibika kwa risala yenye kichwa "Maagizo dhidi ya Wazushi" na, katika sura ya thelathini na sita, aliandika: "Njoni sasa, ninyi mtakaojiingiza katika udadisi ulio bora zaidi, … ambamo ndani yake maandiko yao halisi yanasomwa … Akaya iko karibu nawe sana, (ambamo) unapata Korintho. Kwa kuwa hauko mbali na Makedonia, uko na Filipi; (na huko pia) unao Wathesalonike. Kwa kuwa unaweza kuvuka kwenda Asia, unafika Efeso. Zaidi ya hayo, kwa kuwa wewe ni karibu na Italia, unayo Roma, ambayo kutoka kwake inaingia hata mikononi mwetu mamlaka yenyewe (ya mitume wenyewe)".[8]

Ingawa inakanushwa na baadhi ya wasomi, inathibitishwa na wengine kwamba marejeo hapa ni ya asili ya Kiyunani. Inasemekana kwamba Tertullian anawahimiza wasomaji wake watembelee mahali ambapo maandishi ya awali yanahifadhiwa na hivyo kujionea wenyewe maandishi ya kimungu na matakatifu ya Agano Jipya.[9]

Kunakili Sahihi

Hata iwe hivyo, maandishi ya mitume wenyewe hayangedumu zaidi ya mwaka wa 200 BK. Lakini Bwana wetu alikuwa amedokeza kwamba Maandiko ya Kikristo yangehifadhiwa. "Mbingu na nchi zitapita", Alisema, "lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Mathayo 24:35; taz. 28:20; Marko 8:38; 1 Petro 1:23–25). Bila shaka, uhifadhi wao ulihakikishwa na kunakili kwa uaminifu na kwa uangalifu.

Hata katika nyakati za mitume, nakala za vitabu vya Agano Jipya zilikuwa katika milki ya watu binafsi na ya makanisa. Petro, kwa vyovyote vile, alikuwa anafahamu waraka wa Paulo kwa Wakristo waliokuwa wakiishi Asia Ndogo (Wagalatia, Waefeso, au Wakolosai) na, kwa hakika, anaeleza kwa uwazi kabisa kwamba alikuwa anafahamu "barua [za Paulo] zote" (2 Petro 3:15,16). Kanisa la Kolosai liliambiwa kwamba barua ya Paulo kwao haikupaswa kuchukuliwa kwa maana yoyote kama mali yao ya pekee, lakini – karibu uhakika nakala – ilipaswa "kusomwa pia katika kanisa la Walaodikia". Wakolosai waliambiwa zaidi, "ninyi vivyo hivyo mlisome waraka" – tena, pengine nakala – "kutoka Laodikia" (labda Waefeso; Wakolosai 4:16). Muda si muda, kulikuwa na mikusanyo ya vitabu hivi. Makanisa ya Kikristo yalihitaji seti nzima kwa ajili ya kusoma katika ibada ya hadhara.

Hii inathibitishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja na maandishi ya Mababa wa Kitume katika karne ya pili. Kwa ajili ya ufupi, rejezo laweza kurejezewa kwa mmoja wao tu: Polycarp, mwanafunzi wa mtume Yohana. Akiwaandikia Wafilipi, ananukuu sana kutoka katika Injili na Nyaraka na kisha anaonyesha imani yake kwamba Wafilipi wenyewe "wana ujuzi sana katika Maandiko Matakatifu".[10] Kufikia wakati huu, nakala zilikuwa zimetengenezwa na ushahidi unaonyesha kwamba kusambazwa sana.

Huenda nakala za kwanza zilifanywa na mitume wenyewe. Paulo, katika gereza lake la Kirumi, aliomba aletewe "vitabu, lakini hasa vile vya ngozi" (2 Timotheo 4:13). J.P. Lilley anapendekeza kwamba

““vitabu vya ngozi” vinaweza kuwa nakala au sehemu za Maandiko au hata barua zake mwenyewe kwa Makanisa”.[11] Inafikiriwa pia – na kwa uwezekano fulani – kwamba Yohana alitayarisha nakala saba za “Ufunuo” wake. na kutuma moja kwa kila moja ya makanisa saba ya Asia Ndogo (Ufunuo 1:4–6; 2:1,8,18, n.k.).[12]

Ikiwa mitume wenyewe hawakuwa na jukumu la kunakili sikuzote, basi yaelekea kwamba kazi hiyo mara nyingi ilifanywa na makatibu wao. Tunajua kwa hakika kwamba watu kama hao wakati mwingine waliajiriwa kuandika vitabu au barua (Warumi 16:22; 1 Petro 5:12). Kwa nini wasiungwe mkono kwenye kazi ya kunakili?

“Waandishi”, ambao mwanzoni walikuwa sawa na “makatibu” (Ezra 4:8; Esta 3:12; Yeremia 8:8), walikuwa wameahidiwa kwa Kanisa la Kikristo. “Tazama,” alisema Bwana wetu, “natuma kwenu manabii, na wenye hekima, na waandishi ...” (Mathayo 23:34; taz. 13:52). Tunaweza kudhani kwamba hao walikuwa miongoni mwa wasaidizi wa Paulo. Hakika, mtume anarejelea “Zena mwanasheria na Apolo” (Tito 3:13).

Wanakili walinakili hati hizi kwa uangalifu sana. Tunawezaje kuwa na uhakika kuhusu hili? *Kwanza kabisa*, vitabu hivi vya Agano Jipya viliwekezwa utakatifu sawa na yale ya Maandiko ya Agano la Kale (1 Timotheo 5:18 ambayo inataja Luka 10:7, pamoja na Kumbukumbu la Torati 25:4, kama “maandiko”; na 2 Petro 3:16 ambayo inaweka nyaraka za Paulo katika kundi sawa na “maandiko mengine”). *Pili*, karibu wanakili wote wa mapema wangekuwa waandishi wa Kiyahudi walioajiriwa au walioongoka ambao heshima yao kwa Neno la Mungu lililoandikwa iliwalazimu kujifunza usahihi kamili katika unukuzi (Yeremia 36:28; taz. Kumbukumbu la Torati 10:4). *Tatu*, maandishi yenyewe, yakidai kuwa Neno la Mungu lililovuviwa na lenye mamlaka, yalitoa makatazo makali zaidi dhidi ya aina yoyote ya kuchezea maandishi matakatifu (1 Wakorintho 2:13; 2 Wakorintho 2:17; Ufunuo 22:18,19). *Nne*, wakijua kwamba mitume walikuwa wangali hai na watendaji, wanakili wa mapema wangekuwa waangalifu zaidi kutokeza hati-mkono za ubora wa daraja la kwanza. *Tano*, na hatimaye, ikiwa hapo mwanzo kazi ya kutengeneza nakala ilikabidhiwa kwa watenda kazi wenzi wa mitume ambao walijulikana kama “wainjilisti” (na kulingana na Eusebio lilikuwa ni jukumu lao “kuwapa [waongofu wapya] kitabu cha Mungu. Injili”),[13] yapasa ikumbukwe kwamba watu hawa walipokea vipawa vya kimuujiza vya Roho Mtakatifu na kwa hiyo walikuwa wameandaliwa kwa njia ya pekee kuhifadhi maandishi yaliyopuliziwa (2 Timotheo 1:6, 4:5).

Zaidi ya hayo, kuna jambo la kimungu ambalo halipaswi kupuuzwa. Katika maongozi yake ya usimamiaji na neema, Mungu kwa hakika alihakikisha kwamba maandishi halisi ya Agano Jipya yalipitishwa kwa vizazi vijavyo.

Lahaja katika Maandiko

Licha ya haya yote, makosa yalionekana katika baadhi ya nakala na, kadri nakala zaidi zilipotengenezwa, kulianza kuonekana usomaji wa lahaja kadhaa. Haya kwa kawaida huainishwa kama (1) mabadiliko zisizokusudiwa, na (2) mabadiliko zilizokusudiwa. Aina zisizokusudiwa ni pamoja na maneno yaliyoandikwa vibaya, mkanganyiko wa herufi, mabadiliko ya mpangilio wa maneno, matumizi ya visawe au viambajengo vya maneno, na kuacha au kurudiarudia herufi, maneno, mistari

na hata sehemu. Kwa mbali idadi kubwa zaidi ya lahaja inatokana na kuteleza aina hii kwa upande wa waandishi.

Hata hivyo, Kuna, mabadiliko ya zilizokusudiwa, ambayo kwayo tunamaanisha kuchezea kimakusudi maandishi matakatifu, kwa kawaida kwa maslahi ya theolojia au fundisho fulani. Dionysius, mhudumu wa Korintho, katika barua iliyoandikwa yapata mwaka wa 168–170 BK, anachukizwa na uhakika wa kwamba barua zake mwenyewe zimebadilishwa, kisha aongezea hivi: "Kwa hiyo si ajabu ikiwa wengine wamejiweka wenyewe kuchezea Maandiko Dominika".[14] Mwandishi asiyejulikana (aliyedhaniwa na wengine kuwa Hippolyto, lakini na wengine, Gayo) anaandika mahali fulani karibu mwaka 230 BK: "Wao (wazushi) waliweka mikono bila woga juu ya Maandiko ya Mungu, wakisema kwamba wameyarekebisha".[15] Ni wazushi gani waliothubutu kufanya jambo kama hilo?

Baadhi hawajulikani, kama Asklepiado, Theodoto, Hermophilo, na Apollonido, lakini wengine walijulikana sana kama, kwa mfano, baadhi ya Wagnostiki wa mapema (waliofundisha wokovu kupitia ujuzi wa siri): Basilido, Valentino, na bila shaka Marcioni, ambaye alikubali tu matoleo yake yaliyokatwa ya Injili ya Luka na kumi kati ya nyaraka za Paulo kama kanuni. "Marcioni alitumia kisu kwa uwazi na kwa uwazi, sio kalamu, kwa kuwa alifafanua Maandiko kama inavyofaa mada yake mwenyewe".[16]

Kuirudisha Andiko Halisi la Agano Jipya

Walimu wa Othodoksi walijua kikamili kuhusu mabadiliko hayo maovu, wakiyafichua katika mafundisho yao na katika maandishi yao. Kwa sababu hiyo, hati zilizoonekana kuwa na kasoro kwa jumla hazikutumiwa kwa madhumuni ya kunakili. Ni zile tu ambazo zilihifadhi nakala asili kwa uaminifu zikawa hati za kawaida ambazo nakala nyingi zilifanywa.

Je, tuna ushahidi wowote, hata hivyo, wa kuamini kwamba kweli ndivyo ilivyotokea?

Viongozi wa Wakristo wa mapema kwa hakika walidai uwezo wa kutathmini maandishi mbalimbali na kuamua ni ipi iliyo bora zaidi na sahihi zaidi. Kwa mfano, Irenaeus katika kazi yake kuu ya "Against Heresies" anarejelea "nakala zilizoidhinishwa zaidi na za kale".[17] Aina ya vigezo vilivyotumika kuthibitisha maandishi aminifu vitakuwa kama vifuatavyo:

■ ***1. Utambuzi wa mnakili.*** Ikiwa angekuwa Mkristo wa kawaida, huenda nakala yake ingekuwa na makosa kadhaa. Ikiwa, kwa upande mwingine, alijulikana kuwa msaidizi wa kitume au mwandishi wa kitaaluma, kiwango cha juu sana cha usahihi kingeweza kutarajiwa.

■ ***2. Asili ya muswada ambayo nakala ilitolewa.*** Hapo awali, hii inaweza kuwa nakala asili iliyovuviwa, lakini baadaye ingekuwa yenyewe nakala. Sasa nakala nyingi zilikuwa zile tunazoziita nakala za "faragha": yaani, kama vile zilikusudiwa kwa matumizi ya kibinafsi na ya ibada. Hata hivyo, baadhi zilikuwa nakala "rasmi" ambazo wahudumu Wakristo walisoma na kuhubiri katika huduma za ibada ya hadharani. Hayo ya mwisho yalithibitika kuwa ya kutegemeka zaidi kuliko hizo za kwanza. Nakala zilizotengenezwa kutoka kwa hizi zingeshiriki sehemu kubwa ya kutegemeka kwao.

■ ***3. Idadi ya nakala zilizokuwa zimefanyika.*** Nakala ya nakala asili au mojawapo ya nakala za mwanzo kabisa za nakala halisi itakuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kutoa maandishi yaliyo sahihi kuliko nakala yenye msururu mrefu na tata wa asili. Kwa hiyo, nakala ya zamani zaidi haikuangaliwa, kila mara, kuwa bora zaidi, kwa kuwa huenda ilinakiliwa kutoka kwa nyingine ya kipindi kile kile, ilhali nakala ya baadaye inaweza kuwa ilinakiliwa kutoka ya asili zaidi, karibu na ya asili.

■ ***4. Mahali ambapo nakala ilipatikana.*** Makanisa yenyewe yakawa walinzi wa Neno safi la Mungu (kama ilivyokuwa hapo awali kwa masinagogi ya mitaa); na ikiwa hati iliyonakiliwa ilikuwa imehifadhiwa kanisani, mtu angeweza kuwa na hakika ya kuridhisha kwamba ilikuwa nakala inayotambulika, ya kweli na ifaayo.

■ ***5. Ubora wa jumla wa nakala.*** Baadhi ya nakala zina kasoro dhahiri. Zimeandikwa vibaya na zimejaa makosa ya aina yakupotoka zaidi. Yeyote aliyezitengeneza alikuwa aidha ni mjinga au asiyejali – au, bila shaka, yote mawili. Haya hayangechukuliwa wala kutumiwa kama mashahidi waaminifu kwa maandishi halisi ya Agano Jipya. Hata hivyo, nakala zilizoandikwa kwa uangalifu, zingesisimua ujasiri na, kwa sababu hiyo, zingenakiliwa kwa bidii.

■ ***6. Makubaliano na nakala zingine zilizopo.*** Itakuwa kosa kudhani kwamba mwandishi alikuwa na maandishi moja tu mbele yake. Katika karne mbili za kwanza kulikuwa na mzidisho wa haraka wa nakala, kwa hiyo iliwezekana kwa kulinganisha nakala ili kugundua usomaji usio wa kawaida na, kwa njia iyo hiyo, ili kuhakikisha kile ambacho waandishi waliovuviwa waliandika hasa. Wakristo wa mapema walikuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kufanya hivyo kutuliko sisi. Hata hivyo, walikuwa na uwezo wa kupata maandishi ambayo yamepotea kwa muda mrefu.

■ ***7. Kuwa karibu na kituo kinachojulikana cha Kikristo.*** Nakala iliyofanywa mbali na mahali ambapo mitume na waandamizi wao wa karibu walikuwa wamehudumu mara kwa mara ingekuwa na uwezekano mkubwa wa kupata mabadiliko au marekebisho makubwa; lakini nakala iliyofanywa katika eneo la shughuli za kanisa la awali pengine ingekuwa kiwakilishi cha mapokeo safi ya maandishi.

Walimu wa Kiothodoksi wa karne ya kwanza na ya pili hawakuweza kupata hati bora zaidi kila wakati lakini wanaonekana kujua jinsi ya kutambua "nakala zilizoidhinishwa na za zamani". Kila jaribio lilifanywa kutumia maandishi yao ya msingi, na tokeo lilikuwa kwamba *idadi kubwa sana ya hati za awali za Kiyunani zilikuwa katika makubaliano muhimu*. Kwa hiyo tunaweza kuamini kwamba *maandishi ya wengi yaliwakilisha Maandishi ya Asili kwa usahihi wa kuvutia*.

Hati za Kiyunani zinazosalia

Kulingana na orodha moja ya hivi majuzi, jumla ya hati nzima au sehemu za Agano Jipya ni 5,488.[18] Zimewekwa katika makundi ya kawaida:

□ 1. *Mafunjo.*

Kulingana na takwimu za 1989, kuna 96 kati ya hizi zilizoorodheshwa. Karibu zote ni vipande vipande, ingawa mwanzoni zingetokea katika mfumo wa kodeksi au kitabu. Zimegunduliwa zaidi nchini Misri ambapo hali ya hewa na

mchanga zimesaidia kuzihifadhi. Wanapotaja vipande hivi, wasomi hutumia herufi 'P' ikifuatiwa na nambari ya mfululizo: P1, P2, P3 na kadhalika.

P52 (inayojulikana kama kipande cha Rylands) inachukuliwa kuwa kongwe zaidi. Ina kipimo cha inchi 2 1/2 tu kwa 3 1/2 na ina mistari michache kutoka Injili ya Yohana (18:31–33, 37–38). Ni ya takriban 125 BK.

Miongoni mwa muhimu zaidi ni P45, P46, na P47. Zijulikanazo kama mafunjo za Chester Beatty (baada ya Sir Chester Beatty aliyezipata mwaka wa 1930–1931), hizo zina sehemu za Injili, Nyaraka za Paulo na kitabu cha Ufunuo. Mkusanyiko mwingine muhimu ni mkusanyiko wa Maktaba ya Bodmer (iliyopatikana na M. Martin Bodmer kutoka 1956 na kuendelea). Hii inajumuisha P66, kurasa na vipande kutoka katika kodeksi ya Injili ya Yohana, iliyoandikwa karibu 200 AD; na P72, nakala ya karne ya tatu – na kwa hiyo yawezekana ya mapema zaidi tuliyo nayo – ya Nyaraka za Petro na Yuda.

☐2. *Hati za Maandishi ya Herufi Kubwa.*

Kuna maandishi 299 yanayojulikana. Yaliyoandikwa tangu mwanzoni mwa karne ya nne kwenye ngozi au vellum na katika mfumo wa kodeksi au kitabu, yote yamo katika maandishi ya uncial: yaani, yote yameandikwa kwa herufi kubwa bila alama za uakifishaji. Zile za awali kwa hakika zimeteuliwa kwa herufi kubwa pamoja na nambari za mfululizo zinazoanza na sifuri (k.m., A-02). Baadaye huwa na nambari tu (k.m., 046).

Miongoni mwa walio katika Jumba la Makumbusho la Uingereza ni Kodeksi Alexandrinus, A-02. Kitabu hiki kilinakiliwa huko Misri katika nusu ya kwanza ya karne ya tano na, kilipokamilika, kilikuwa na Biblia nzima ya Kiyunani pamoja na kitabu kimoja au viwili vya apokrifa. Sasa ina takriban Agano la Kale lote na sehemu kubwa ya Agano Jipya (ukiondoa Mathayo 1:1–25:6; Yohana 6:50–8:52; 2 Wakorintho 4:13–12:7). Baba wa Alexandria aliwasilisha hati hii kwa Charles I mnamo 1627.

Kodeksi nyingine ambayo ni ya karne ya tano ni Kodeksi Bezae, D05. Mnamo 1581, Theodore Beza, mrithi wa John Calvin, aliwasilisha hati hii kwa Chuo Kikuu cha Cambridge ambapo bado iko. Kodeksi hii ina maandishi ya Kigiriki na Kilatini (ukurasa wa kushoto katika ukurasa wa kwanza, wa kulia katika wa mwisho) na ina vitabu vingi vya Injili na Kitabu cha Matendo, pamoja na mistari michache kutoka 3 Yohana.

Maarufu zaidi kati ya maandishi ya kwanza ni Kodeksi Sinaiticus, Aleph-01 (Aleph ikiwa herufi ya kwanza ya alfabeti ya Kiebrania), na Kodeksi Vaticanus, B-03.

Kodeksi nyingine ambayo ni ya karne ya tano ni Kodeksi Bezae, D05. Mnamo 1581, Theodore Beza, mrithi wa John Calvin, aliwasilisha hati hii kwa Chuo Kikuu cha Cambridge ambako bado iko. Kodeksi hii ina maandishi ya Kigiriki na Kilatini (ukurasa wa kushoto ikiwa hiyo ya awali, na, wa kulia ikiwa hiyo ya mwisho) na ina karibu Injili yote na Kitabu cha Matendo, pamoja na mistari michache kutoka 3 Yohana.

Maarufu zaidi kati ya hati za maandishi makuu ni Kodeksi ya Sinai, Aleph-01 (Aleph ikiwa herufi ya kwanza ya alfabeti ya Kiebrania), na Kodeksi ya Vatikani, B-03.

Kodeksi ya Sinai, iliyoandikwa katikati au mwisho wa karne ya nne, ina sehemu tu ya Agano la Kale lakini Agano Jipya lote la Kiyunani. Ndiyo hati kamili ya maandishi makuu ya Agano Jipya iliyopo. Kodeksi hii ya Misri iliandikwa kwenye ngozi, ikiwa na safu nne za mistari arobaini na minane kwenye kila ukurasa, lakini kuna dalili za wazi katika maandishi yenyewe kwamba imesahihishwa mara kadhaa. Katika mwaka wa 1844 Constantine Tischendorf aligundua baadhi ya kurasa zake katika kikapu cha karatasi taka katika maktaba ya monasteri ya Mt. Catherine kwenye Mlima Sinai. Ilimbidi angoje hadi 1859, hata hivyo, kabla ya kuona Agano Jipya lote. Baada ya kupata ruhusa, aliihamisha Cairo ambako alitoa nakala yake; na mnamo 1862, kupitia ukarimu wa Alexander II, Mfalme wa Urusi, alichapisha toleo la maandishi hayo yenye Utangulizi na Vidokezo muhimu.

Kodeksi ya Vatikani inaweza pia kupewa tarehe ya katikati ya karne ya nne na, kama Aleph, imeandikwa kwenye ngozi laini lakini ikiwa na safu tatu kwenye ukurasa, kila moja ikiwa na mistari arobaini na miwili. Ikiwa ni Biblia kamili ya Kiyunani hapo awali, sehemu za Agano la Kale na sehemu kubwa kadhaa za Agano Jipya zimekuwa zimepotea kwa muda sasa. Zinazokosekana kutoka kwenye hati hii ya maandishi makuu ni Nyaraka za Kiuchungaji, Filemoni, hitimisho la Waebrania (9:14 hadi mwisho), na kitabu kizima cha Ufunuo. Wasahihishaji mbalimbali wamekuwa wakifanya kazi katika maandishi hayo na, katika karne ya kumi, mtu fulani alifuatilia sehemu kubwa ya maandishi ya awali, akihofia, kwamba herufi zake zingeweza kufifia. Sifa za kipekee za tahajia zinapendekeza asili ya Kialeksandria lakini hakuna anayejua ilikuja aje katika Maktaba ya Vatikani huko Roma. Maktaba hii ilianzishwa mwaka 1448 na Papa Nicolas V na hati hii imeorodheshwa katika katalogi ya kwanza kabisa, iliyotolewa mwaka wa 1475. Samuel Tregelles alijaribu kuitazama mwaka 1845 lakini alizuiliwa sana na walezi wake wa makasisi. Mnamo 1866, Tischendorf alipewa ruhusa ya kuisoma kwa saa arobaini na mbili na, kutokana na utafiti wake na maelezo yake, toleo la mswada huu – Kodeksi B – lilitolewa mnamo 1867. Hili lilifuatiwa na toleo lililotolewa na mamlaka ya Papa na kutayarishwa na Vercellone. na Cozza mwaka 1868; na, basi, katika 1889–90, faksi ya picha ilitolewa kwa wasomi.

▫3. *Maandishi ya Herufi Ndogo.*

Kuna 2,812 kati ya hizi. Zinaitwa za herufi ndogo kwa sababu zimeandikwa si kwa herufi kubwa lakini kwa herufi ndogo (zinazoitwa “miniscules” au herufi mlazo). Mtindo huu wa uandishi ulikuwa umetumika kwa karne nyingi katika hati za kibinafsi lakini haikuwa hadi karne ya tisa ambapo ulitumiwa kwa madhumuni ya kifasihi. Huku mahitaji ya vitabu vya Agano Jipya yakizidi kuongezeka, hati hii ilikuwa na manufaa ya kuchukua muda mfupi kuandika na kuchukua nafasi kidogo kwenye ngozi. Kwa madhumuni ya kitambulisho, huteuliwa na nambari za kawaida (1,2,3 na kadhalika).

Herufi ndogo, basi, ziliandikwa kuanzia karne ya tisa na kuendelea; lakini tarehe zao za baadaye haimaanishi kuwa hizo ni shahidi zisizoaminika sana za asili. Hati za karne ya tisa zinaweza kuwa zilinakiliwa kutoka kwa zingine za karne ya tatu. Kama Profesa Warfield alivyowahi kuona, “Si idadi tu ya miaka ambayo iko nyuma ya hati. ambayo hupima umbali wake kutoka kwa za asili, lakini idadi ya nakala”.[19]

Hati za herufi ndogo hizi ni pamoja na zifuatazo:

MS 1: kodeksi ya karne ya kumi na mbili, yenye Agano Jipya lote, kasoro kitabu cha Ufunuo. MS 4: nakala ya karne ya kumi na mbili ya Injili nne. MS 12: nakala ya Injili ya karne ya kumi na moja. MS 21: kutoka karne ya kumi lakini pia iliyo na Injili. MS 43: kazi ya karne ya kumi na moja katika juzuu mbili, ya kwanza ikiwa na Injili na ya pili, Matendo na Nyaraka. MS 330: karne ya kumi na moja, iliyo na Injili, Matendo, na Nyaraka. MS 565: nakala nzuri sana ya karne ya tisa ya Injili, iliyoandikwa kwa herufi za dhahabu kwenye ngozi ya zambarau.

❑4. *Hadhara.*

Yakiwa ni 2,281, haya ni maandishi ya mapema kama tangu karne ya sita, yenye Injili na Nyaraka.

(Evangeliaria na Apostoli) iliyoteuliwa kusomwa katika makanisa ya kwanza ya Kikristo. Nyingi zao hutumia herufi zisizo za kawaida lakini zingine ni za herufi ndogo; na, kwa mara nyingine tena, uteuzi ni kwa nambari lakini wakati huu zimewekwa kiambishi awali na 'l' au kwa ufupisho 'Lect' (k.m., l59 au Lect. 1280).

Haya ni maandishi muhimu, si tu kwa sababu baadhi yake ni ya mapema, bali pia kwa sababu zilitumika kwa kusomwa katika ibada za hadhara za Kanisa. *Uangalifu mkubwa zaidi ingechukuliwa juu ya nakala hizi za kanisa ili kuhifadhi usafi wao wa asili; na ushuhuda wa mhadhara* ungekuwa, kwa hakika, *ushuhuda wa makanisa yote*. Sasa, Mahadhiri zilizosalia ambazo zimechunguzwa zinapatikana kukubaliana kwa kiwango cha kushangaza. Maelezo pekee ya kuridhisha, kwa hakika, ni kwamba kulikuwa na *maandishi ya mhadhara yanayotambulika*.

Uainishaji

Idadi kubwa ya hati za Kiyunani kwa hiyo zinapatikana kwetu, zilizoandikwa tangu mapema kama karne ya pili hivi. Wasomi waliozisoma wanashikilia kwamba, ingawa kuna lahaja, hati fulani ina usomaji mwingi unaofanana ambayo inaonyesha kuwa kuna vikundi au familia. Aina kuu za maandishi ni kama ifuatavyo: (i) ya Kibizantini (wakati mwingine huitwa maandishi ya Jadi, ya Wengi, au ya Kiantiokia); (ii) ya Kialeksandria (au ile ambayo wengine wameiita Maandishi yasiyo ya upande wowote); (iii) ya Kimagharibi; na (iv) ya Kikaisaria.

Kwa madhumuni ya makala haya, aina mbili za mwisho za maandishi hazihitaji maoni ya kina. Ilikuwa B.H. Streeter, katika *Injili Nne* (1924), ambaye kwanza alidai kuwa amepata maandishi ya Kikaisaria. Aliamini kwamba hii ilikuwa ni andiko la Injili ya Marko ambalo Origen alinukuu baada ya 231 AD, mwaka baada ya kufika Kaisaria. Wahakiki wa kisasa wa maandishi, hata hivyo, wana shaka ikiwa hii inaweza kweli kuitwa aina tofauti ya maandishi. Wao huwa badala yake hufikiria kuwa ni mchanganyiko tu.

Na kuhusu aina ya maandishi ya Kimagharibi, iliyotambuliwa na B.F. Westcott na F.J.A. Hort, na ikifikiriwa kuwa asili yake ni Ulaya Magharibi, kungeonekana kuwa na ushahidi *fulani* wa kuwepo kwake. Inawakilishwa na Kodeksi Bezae (karne ya tano), Kodeksi Claromontanus (karne ya sita), na tafrisir za Kilatini cha Kale na Curetonian ya Kisiria (karne ya tatu na ya tano mtawalia). Pia imenukuliwa na baadhi ya Mababa wa Kanisa wa mapema, kama vile Irenaeus,

Tertullian, na Cyprian. Walakini, aina hii ya maandishi mara nyingi ni tofauti kabisa na zingine zote. Imegubikwa na kasoro kadhaa, sio tu za aya bali pia vifungu vizima. Mwelekeo wake unaotawala, hata hivyo, ni wa kufanya nyongeza, ama kwa njia ya kufafanua au kwa kuingiza maelezo ya ziada. Katika Injili (hasa katika sehemu ya mwisho ya Injili ya Luka) ni fupi zaidi, wakati katika Matendo ni mrefu zaidi (takriban 10% zaidi). Sir Frederic Kenyon aliielezea kama "aina ya maandishi yenye sifa ya kuondoka kwa uhuru kutoka kwa mapokeo ya kweli". Upungufu wa uthibitashii wa hati, pamoja na wingi wa utofauti katika usomajii, hufanya aina hii ya maandishi kwa ubora wake kuwa ya kutiliwa shaka, na kwa ubaya wake, kuwa ya kutoaminika kabisa.

Hii kweli inatuacha na vikundi viwili vikubwa vya maandishi: ya Kibizantini na ya Kilexandria.

◻A. *Maandishi ya aina ya Kibizantini*

Nakala hii inapokea jina lake kutokana na ukweli kwamba ilihusishwa mapema na mji mkuu wa kifalme wa Constantinople, ambayo zamani iliitwa Byzantium, na pia kutokana na ukweli kwamba ikawa maandishi ya kawaida ya Kanisa la Kikristo katika kipindi chote cha Byzantine, 312–1453 BK (na. kwa kweli muda mrefu baada ya hapo). Hata hivyo, kabla ya kutawazwa kwalo katika jiji kuu la Mashariki, aina hii ya maandishi ilikuwa imehifadhiwa katika Antiokia, mji mkuu wa mkoa wa Kiroma wa Siria. Ni wazi kuwa Waalimu wa Kikristo wahusishwao na kanisa la huko waliitumia. Hawa ni pamoja na Basil wa Kaisaria, Gregory wa Nyssa, Gregory wa Nazianzus (Mababa wa Kapadokia), Theodoret wa Koreshi, na Chrysostom wa Constantinople (aliyehama kutoka Antiokia na kuwa askofu wa Constantinople mwaka wa 398 BK).

Aina ya maandishi ya Kibizantini ina *uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa hati za Kiyunani*.

Katika mafunjo ya mapema kuna idadi ya kuvutia ya usomaji wa Kibizantini. P45 na P46 za Chester Beatty Papyri zina usomaji kama huo, kama pia P66 ya mkusanyiko wa Maktaba ya Bodmer. Profesa H. A. Sturz aliweza kuorodhesha usomaji *150 wa Byzantine kwa usaidizi wa mapema wa mafunjo*.[20] Hii inaonyesha wazi kwamba, kinyume na maoni ya wahakiki wa maandishi wa awali, usomaji wa Kibizantini unaweza kufuatiliwa hadi karne ya pili.

Miongoni mwa maandishi ya herufi kubwa, maandishi haya yanapatikana katika Kodeksi ya karne ya tano ya Alexandrinus (A-02; Byzantine katika Injili), na Ephraemi (C-01), na kwa hakika zote za baadaye. Inakadiriwa kuwa takriban 95% ya maandishi ya herufi kubwa yana aina ya maandishi ya Kibizantini. Hata zaidi inaweza kudaiwa kwa Minuscules, kwa kuwa karibu zote hizi ni za Kibizantini katika usomaji wao. Vitabu vilivyochunguzwa hivi sasa vinaunga mkono aina ya maandishi ya Kibizantinie.

Mihadhiri zilizochunguzwa hata sasa pia vinaunga mkono aina ya maandishi ya Kibizantini.

◻ *1. Uungwaji mkono na matoleo ya awali*

Hizi zilikuwa tafsiri za mwanzo za Maandiko ya Agano Jipya, zilizotayarishwa kusaidia kueneza Imani ya Kikristo kati ya watu wa ulimwengu. Miongoni mwa

matoleo ya awali tunayoyajua ni Matoleo ya Kisiria (au Kiaramu) na Kilatini ambayo yanarudi katikati ya karne ya pili. Peshitta, "Malkia wa Matoleo", ni mojawapo ya tafsiri za awali za Kisiria na kwa hakika ina usomaji wa Kibizantini. Hii pia ni kweli kuhusu toleo la Kigothi la karne ya nne, linalosemekana kutafsiriwa na Ufilas, askofu wa Antiokia.

2. *Kuthibitishwa na Mababa wa mwanzo*

Wachambuzi wanaokana ukuu wa maandishi ya Kibizantini, wakipendelea kuyaona kuwa masahihisho ya karne ya nne, mara nyingi hurejelea ukweli kwamba hakuna Baba wa Kanisa la Mapema kabla ya Chrysostom (347–407 BK) anayeonekana hata kuirejelea, sembuse kunukuu kutoka kwayo. Sasa hii sio kweli. Utafiti wa kina wa kitaalamu umeonyesha kuwa Justin Martyr (100–165 BK), Irenaeus (130–200 BK), Clement wa Alexandria (150–215 BK), Tertullian (160–220 BK), Hippolytus (170–236 BK), na hata Origen (185–254 BK) ananukuu mara kwa mara kutoka kwa maandishi ya Kibizantini. Edward Miller, baada ya kuainisha manukuu katika Mababa wa Kiyunani na Kirumi waliokufa kabla ya 400 BK, aligundua kwamba manukuu yao yaliunga mkono maandishi ya Kibizantini mara 2,630 (na maandishi mengine mara 1,753 tu). Zaidi ya hayo, akichunguza vifungu thelathini muhimu, alipata ushuhuda 530 kwa maandishi ya Kibizantini (na 170 tu kwa ajili ya wapinzani wake). Hili ndilo lilikuwa hitimisho lake: "Utawala asilia wa Maandishi ya Jadi umeonyeshwa katika orodha ya Mababa wa awali. Kumbukumbu zao zinathibitisha kwamba katika maandishi yao, na hivyo katika Kanisa kwa ujumla, ufisadi ulijifanya kuhisiwa katika nyakati za awali, lakini kwamba maji safi kwa ujumla yalitawala … Mapokeo hayo pia yanaendelezwa kupitia kwa Mababa walio wengi waliowafuata. Hakuna mapumziko au muda: shahidi ni mwenye kuendelea".[21]

Ukweli ulio wazi wa jambo hilo ni kwamba kufikia karne ya nne maandishi ya Byzantium yalikuwa yakitokea kama maandishi ya Agano Jipya yenye mamlaka na kwa miaka elfu moja na mia mbili iliyofuata (na zaidi) yalishikilia mamlaka isiyopingwa juu ya Jumuiya yote ya Kikristo.

3. *Agano Jipya la Kiyunani Lililochapishwa*

Agano Jipya la Kiyunani lilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1514, ingawa halikuchapishwa katika toleo tofauti hadi 1522. Hiyo ilikuwa kazi ya Francisco Ximenes, Kardinali kiongozi wa Uhispania, nayo ilikuwa sehemu ya vitabu vyake sita "Complutensian Polyglot". Katika Wakfu wake kwa Papa Leo wa Kumi, Ximenes aliandika hivi: "Kwa nakala za Kiyunani kwa hakika tuna deni kwako Baba Mtakatifu, ambaye ulitutumia kwa fadhili zaidi kutoka katika Maktaba ya Kitume kodeksi za kale sana, zote za Agano la Kale na Jipya; ambayo yametusaidia sana katika shughuli hii". Maandishi ya matokeo ya Kiyunani yanaonekana kuwa ya aina ya Kibizantini (na hakuna uthibitisho kwamba Ximenes aliwahi kufuata Kodeksi ya Vatikani [B]).

Mnamo mwaka wa 1516, Desiderius Erasmus, msomi mashuhuri zaidi katika Ulaya, alipochapisha chapa ya kwanza ya Agano Jipya la Kiyunani, aliitegemea hati za Kibizantini. Erasmus alitoa matoleo mengine manne ya kazi yake, mwaka wa 1519, 1522, 1527, na 1535. Upesi wengine walifuata nyayo zake: hasa Robert Estienne

(aliyeitwa Stafano kwa Kirumi), mhariri na mchapishaji Mfaransa, ambaye maandishi yake yaliyochapishwa katika 1546 yalikuwa sawa na ile ya Erasmus. Kulikuwa na matoleo matatu yaliyofuata katika 1549, 1550, na 1551. Bado matoleo zaidi yalihaririwa na kuchapishwa na Theodore Beza kati ya 1565 na 1604. Kisha, katika 1624, Bonaventure na Abraham Elzevir wakatoa chapa yao. Dibaji ya toleo la pili la Elzevirs, iliyochapishwa mnamo 1633, ina maneno haya: "Kwa hivyo unayo maandishi ambayo sasa yamepokelewa na wote, ambayo ndani yake hatutoi mabadiliko au ufisadi". Kutoka kwa hili likaja jina linalojulikana sasa "*Nakala Pokelezi*".

Maandishi ya Kibizantini yalikuwa *maandishi ya msingi ya Biblia zote kuu za Kiingereza za Kiprotestanti*, ikijumlisha zile zilizohusishwa na majina ya William Tyndale (1525), Miles Coverdale (1535), John Rogers (1537), na Richard Taverner (1539), pamoja na zile zinazojulikana kuwa Biblia Kuu (1539), Biblia ya Geneva (1560), Biblia ya Maaskofu (1568), na, bila shaka, Toleo Idhinishi (1611); na lile la Reina katika Kihispania, la Karoli katika Kihungari, Luther katika Kijerumani, Olivetan katika Kifaransa, Statenvertaling katika Kiholanzi, Almeida katika Kireno na Diodati katika Kitaliani.

Kwa muhtasari hapa, hoja zinazounga mkono maandishi ya Kibizantini ni kama ifuatavyo.

■1. Aina hii ya maandishi *yahusishwa na mji wa Antiokia huko Syria*. Baada ya kifo cha Stefano, Wakristo kutoka Yerusalemu walikimbilia mji huu na kuanza kuhubiri Injili kwa Waayunani huko (Matendo 11:19,20). Kanisa imara lilitokea, kwa kiasi kikubwa kupitia huduma za Barnaba na Paulo (11:22–26), na kutoka kanisa hili mtume alianzia kila safari yake ya kimishonari (Matendo 13:1–3, 15:35,36; 18:22,23). Mitume wengine walitembelea mahali hapo, akiwemo mtume Petro (Wagalatia 2:11,12). Haikupita muda mrefu kabla ya Antiokia kuwa mji mama kwa makanisa ya Kimataifa na, baada ya kuanguka kwa Yerusalemu mwaka wa 70 BK, ikawa kitovu cha kweli cha Ukristo kisichopingika. Andiko linalotoka Antiokia lingekuwa andiko lililoidhinishwa na mitume na Kanisa la Kikristo la mapema.

■2. Kama ambavyo tayari imeonekana, andiko hili lilipokea jina lake kutoka Konstantinople (Bizantini), mji mkuu wa Milki ya Mashariki, kwa sababu lilithibitishwa huko mapema kama maandishi pimika ya Kiyunani. Konstantinople ilikuwa kitovu cha ulimwengu wa watu wanaozungumza Kiyunani na Kanisa linalozungumza Kiyunani, kwa kuwa katika nchi za Magharibi, Kiyunani kilikuwa kimeachia Kirumi nafasi, huko Mashariki, kilikuwa kimebaki kuwa lugha rasmi na ya kawaida. Hilo lilimaanisha, bila shaka, kwamba *wasomi wa Kiyunani katika Konstantinople walifaa kwa njia ya pekee kutambua na kutoa maandishi hayo halisi*.

■3. *Wakati wa karne ya nne wakati andiko hili lilikuwa kuu, Kanisa lilibarikiwa kuwa na wasomi wa kipekee* kama vile Methodio (BK 260–312), Athanasio (296–373), Hilary wa Poitieri (315–67), Cyril wa Yerusalemu (315–386), na Gregory wa Nazianzeni (330–394). Watu hawa – na wengine kama wao – walihusika katika kuunda fundisho halisi na kuridhia kanuni za Agano Jipya. Pia walijitolea kusoma maandishi; na walikuwa na faida zaidi ya wakosoaji wa baadaye kwa sababu ya uweza wao wa kufikia maandishi mengi ya mapema na yenye thamani sana ambayo yamepotea tangu zamani. Kuibuka kwa

maandishi kuu kutoka kwa kipindi hiki ni muhimu sana. Ni dhahiri ilizingatiwa kuwa maandishi halisi, yasiyopotoshwa, na yaliyoidhinishwa.

■4. Wayahudi waliwekwa kuwa walinzi wa mafunuo ya kimungu waliyopewa na, katika kutimiza amana walio wekewa, walihifadhi kwa uangalifu maandishi ya Agano la Kale bila kupotoshwa na nzima (maandishi ya Kiebrania ya Kimasoreti). Kama vile mtume Paulo alivyoashiria, "kwao yaliwekwa maneno ya Mungu" (Warumi 3:2). Sasa ni jambo la busara kudhani kwamba *Maandiko ya Agano Jipya yalipewa kwa wanaokiri kuwa Wakristo, au kwa wale wanaokiri kuwa Kanisa la Kikristo*. Swali ambalo kwa kawaida hujitokeza ni: Ni aina gani ya maandishi, kwa ujumla, ambayo imetambuliwa na kuenezwa na Kanisa tangu nyakati za awali? Jibu ni: aina ya maandishi inayojulikana kama ya Kibizantini.

■5. Ukweli ni kwamba takriban 90% ya maandishi ya Kiyunani yanawakilisha aina ya maandishi ya Kibizantini. Ingawa hati hizi si za mapema kama vile baadhi ya wakosoaji wangependa, ni nyingi sana hivi kwamba ni lazima tuchukulie kwamba kulikuwa na mamia ya hati-za-kizazi nzee, nyingi zikiwa za nyakati za mapema zaidi za Ukristo. Kwa namna fulani ukweli huu unapaswa kuelezwa; na hairidhishi hata kidogo kuendelea kubishana – dhidi ya ushahidi unaoongezeka – kwamba maandishi ya Kibizantini hayaonekani katika historia hadi karne ya nne. Nakala hii ni ya mapema. Ilienea sana kwa sababu iliwakilisha kwa uaminifu ile ya asili.

■6. *Utunzaji kimajaliwa umekuwa kila mara kuelekea Kweli ya Mungu, kwa sababu waamini wamehitaji Ukweli huo katika uhakika na usahihi wake* (Mathayo 24:35; 1 Petro 1:23,25). Kwa hiyo, Neno lililotolewa kwa uvuvio limekuwa sawa na lile lililochapishwa baadaye (Zaburi 68:11). Haiwezekani kuwaza kwamba Mungu angewapa watu wake maandishi yaliyopotoka na yaliyoharibika kabisa na kisha kuruhusu maandishi hayo kutumiwa nao kwa zaidi ya karne kumi na nane. Lakini hivyo ndivyo wakosoaji fulani wa maandiko wa kisasa wangetaka tuamini! "Ikumbukwe", anaandika Dkt. Owen, "kwamba nakala kawaida tunayotumia (Nakala Pokelezi) ilikuwa milki ya umma ya vizazi vingi … basi hilo lipite kuwa kiwango, ambacho bila shaka ni haki na kustahili, nasi, Mungu akisaidia, tutaona upesi jinsi kuna sababu ndogo ya kujifanya aina za usomaji kama hizi ambazo sasa tunashangazwa nazo".[22]

■7. Ni jambo la busara kudhani kwamba *Mungu alitenda visawa kuhusiana na maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya*. Mbinu yake na Agano la Kale ilikuwa kuhifadhi maandishi, katika hali ambayo haijabadilishwa, kupitia vizazi vingi. Matokeo yake – jinsi Kristo na mitume wake walivyofundisha – kilikuwa Kitabu ambacho kila herufi na sehemu ya herufi ilikuwa takatifu (Mathayo 5:18; taz. Yohana 10:35). Wakati ufunuo huu wa kale ulipoongezewa, Mungu aliendelea kwa njia ile ile: Aliandika Neno Lake la hivi punde bila kosa, akaliweka katika milki ya Kanisa Lake, na kisha *kuhakikisha kwamba lilipitishwa kupitia karne zilizofuata, hata hadi wakati huu wa sasa*. "Neno la Bwana … linaloshi na linalodumu milele" (1 Petro 1:25).

□B. Aina ya Maandishi ya KiAlexandria

■ Hiki ni kikundi kidogo sana cha maandishi. Sifa za kipekee za tahajia zinaonyesha kwamba zinapaswa kuhusishwa na

Alexandria huko Misri; na, haishangazi, usomaji kutoka kwa aina hii ya maandishi unapatikana kati ya funjo za kiMisri za mapema (kwa mfano, P46, P47). Hata hivyo, wawakilishi wake wakuu ni Kodeksi ya Sinaiticus (au Kodeksi Aleph) na Kodeksi Vaticanus (au Kodeksi B).

Uungwaji wa aina hii ya maandishi unatoka kwa Mababa wa kiAlexandria, haswa kutoka kwa Origen (AD 185–254) na Cyril (376–444).

Mambo kadhaa yanapaswa kuzingatiwa hapa:

■1. Aina hii ya maandishi *ilitoka Alexandria, huko Misri*. Maandiko hayaonyeshi kama kumewahi kuwa na uwepo wa mitume katika sehemu hizo, lakini historia ya kanisa inonyesha kwamba wazushi wengi wenye sifa mbaya waliishi na kufundisha huko wakiwemo Wagnostiki kama Basilides, Isidore, na Valentinus. Chochote kinachotokea kutoka mahali hapa lazima kiangaliwe kwa tuhuma fulani.

■2. Kuna *ushahidi wa wazi wa urekebishaji* katika upangaji wake upya wa maneno. B.H. Streeter alipendekeza kwamba mhariri alikuwa askofu wa Misri anayeitwa Hesychius.[23] Hii ina maana kwamba ingawa madai makubwa yanatolewa kwa ajili yake, aina hii ya maandishi haiwezi kuzingatiwa kwa umoja kama "safi".

■3. Wawakilishi wawili wakuu wa aina hii ya maandishi, Kodeksi za Aleph (Sinaiticus) na B (Vaticanus) *ni duni sana katika ubora*. Ilipochunguzwa na Dk. F.H.A. Scrivener, Kodeksi Aleph ilitangazwa kuwa "imeandikwa vibaya" na "imejaa makosa makubwa ya kimaandishi" kama vile "kuacha mistari yote ya asili". Kodeksi B, ingawa kwa ulinganifu "ilikuwa na dosari kidogo", ilipatikana kuwa "inawajibika kukosea" ikiwa na "makosa ya kitabia yanaonekana zaidi".[24]

■4. Hati hizi kuu zinaonyesha upotovu wao kwa *kutokubaliana wao wenyewe katika maelfu ya sehemu* (mara 3,000 katika Injili pekee).

■5. Andiko lililothibitishwa na Aleph (Sinaiticus) na B (Vaticanus) *yatofautiana na mengi kati yamaandishi Kiyunani*. Sio tu kwamba imefungwa kwa familia ndogo sana ya maandishi, lakini imekadiriwa kwamba kuna mahali fulani katika eneo la tofauti 6,000 kati ya maandiko ya kiAlexandria na Kibizantini.

■6. Ni kweli kwamba kuna upotevu mkubwa wa maandishi katika B (Vaticanus), lakini kwa kuzingatia umri yake (katikati au mwishoni mwa karne ya nne), maandishi haya mawili ya herufi kubwa yamo katika hali nzuri sana. Kwa kuwa maandishi mengi sahihi ya wakati huu yalipotea kwa sababu ya matumizi, inaweza kudhaniwa kwamba haya *yalikataliwa kama yenye dosari na kwa hivyo hayakutumiwa na kanisa la kwanza*.

■7. Kuunga mkono hitimisho hili ni ukweli kwamba *nakala chache sana zilifanywa kutoka kwao*. Kama ilivyoelezwa na Dkt. Gordon Clark, "Ikiwa hati moja au mbili zina babu mmoja, inadokeza kwamba mnakili mmoja au wawili waliamini kwamba hati hiyo ilikuwa aminifu kwa maandishi. Lakini ikiwa hati haina wazao wengi, kama ilivyo kwa babu wa B, mtu anaweza kushuku kwamba waandishi wa mapema walitilia shaka thamani yake. Yamkini Wakristo wa awali wa kiorthodoksi walijua kwamba B ilikuwa potovu."[25]

Wakosoaji Washambulia Maandiko ya Kibizantini

Katika karne iliyopita, wasomi wawili wa Cambridge, B.F. Westcott na F.J.A. Hort, *walifafanua nadharia mpya kali* kuhusu uwasilishaji wa mapema wa maandishi ya Agano Jipya. Walibishana kwamba maandishi bora zaidi yalikuwa ya Kialeksandria (waliyoyaita "Maandiko Yasio na Upande wowote") yakiwakilishwa na Aleph na B. Kwa kuwa maandishi hayo mawili yalikuwa ya mapema kidogo kuliko mengine, walidai kwamba babu yao wa kawaida alikuwa karibu na asili iliyovuviwa. Ingawa usafi kamili haukuhusishwa na maandishi haya, Westcott na Hort walikuwa tayari kusema, "Ni imani yetu (1) usomaji wa Aleph B unapaswa kukubaliwa kama usomaji wa kweli hadi uthibitisho wenye nguvu wa ndani upatikane kinyume chake, na (2) kwamba hakuna usomaji wowote wa Aleph B unaoweza kukataliwa kwa usalama kabisa, ingawa wakati mwingine ni sawa kuyaweka kwenye msingi mbadala, hasa pale ambapo hayapati msaada wowote kutoka kwa Matoleo au Mababa".[26]

Maandishi ya Kibizantini (inayoitwa "Maandishi ya kiSyria") yalikuwa na, kama walivyofikiri, "Usomi Changanyiko", yaani, mchanganyiko wa masomo ya awali; na waliamini yalianzia katika marekebisho ya hatua mbili yaliyotolewa huko au karibu na Antiokia katika karne ya nne. Wakikubali kuwa hii ni "dhana" tu, waliendeleza maoni kwamba "utofauti unaokua na mkanganyiko wa maandishi ya Kiyunani ulisababisha kusahihishwa kwa mamlaka huko Antiokia" na baadaye "kwenye marekebisho ya pili ya mamlaka". Mchakato mzima, kwa mujibu wao, ulikamilika mwaka 350 BK; na hata waliweka pendekezo kwamba Lucian wa Antiokia (aliyeuawa kishahidi mwaka 312) anaweza kuwa alihusika katika marekebisho ya awali.

Nadharia hiyo ina dosari kubwa. Ingawa wakosoaji na matoleo bado yanarejelea "hati za kale zaidi na bora zaidi", kifungu hicho kinapotosha kabisa kwa sababu, katika mjadala huu mahususi, "zamani" kwa kweli ni "mbaya zaidi". Kuhusu "masomo ya pamoja" katika maandishi ya Byzantine, ushahidi wa kusadikisha unaounga mkono haujawahi kutolewa (hata baada ya miaka ishirini na minane ya masomo Westcott na Hort wangeweza kutoa mifano minane tu). Hata hivyo, usomaji wa muda mrefu hauthibitishi kuingiliwa baadaye kwa maandishi. Profesa Sturz ameonyesha kwamba baadhi ya usomaji huu unaungwa mkono na mafunjo ya awali zaidi (somo refu zaidi la Yohana 10:19 na 10:31, kwa mfano, linaungwa mkono na P66).[27] Hii inaongoza kwenye hitimisho kwamba kosa liko kwa Maandishi ya kiAlexandria. Inashutumiwa kwa kufupisha maandishi ya Kibizantini. Je, basi kuhusu kile kinachojulikana kama "Lucianic Recension"? Hakuna ushahidi kwamba iliwahi kutokea.

Westcott na Hort walianza kazi ya kutayarisha maandishi ya Kiyunani yaliyorekebishwa. Inatokea kwamba wao pia walikuwa washiriki wa kamati, iliyoteuliwa na Kongamano la Canterbury mnamo 1880, kutayarisha toleo lililosahihishwa la Biblia ya Kiingereza. Ingawa maandishi yao ya Kiyunani yalikuwa bado hayajachapishwa, nakala ya uthibitisho ilitolewa kwa wasahihishaji; na katika 1881 Agano Jipya la Toleo Iliyorekebishwa lilipotokea, ilionekana wazi mara moja kwamba maandishi ya Kiyunani ya Westcott na Hort hayakuwa tu na uvutio mkubwa kwenye halmashauri hiyo bali pia yalikuwa yamefuatwa kwa

ujumla katika Toleo Iliyorekebishwa ya Agano Jipya la Kiingereeza.

Andiko hili la Westcott/Hort lilikuwa mtangulizi wa kile kinachojulikana leo kama Nestle/Aland (United Bible Societies). Maandishi, ambayo yamenyakua nafasi ya Maandishi ya Kibizantine au Jadi na hatimaye kuunda msingi wa takriban matoleo yote ya kisasa. Kwa kielelezo, New International Version, ingawa katika utangulizi wake inadai kufuata maandishi ya Kigiriki 'eclectic' (yaani, moja iliyokusanywa kutoka katika maandishi mbalimbali), inaendelea mara moja kumjulisha msomaji kwamba "ambapo hati zilizopo zinatofautiana, watafsiri walifanya uchaguzi wao wa usomaji kulingana na kanuni zinazokubalika za uhakiki wa maandishi wa Agano Jipya". Kupitishwa kwa 'kanuni' zenye kasoro kimsingi kumemaanisha kwamba maandishi tokeo yanafanana sana na yale yaliyotolewa mwaka wa 1881 na Westcott na Hort.

Toleo Lililoidhinishwa

Wakati wa kipindi cha Marekebisho ya Kidini na Wapuritani, matoleo kadhaa ya Kiprotestanti yalitokezwa, yote yakitegemea maandishi yaleyale ya kweli na kutafsiriwa kulingana na kanuni zilezile zinazofaa.

Mnamo 1611, Toleo Lililoidhinishwa lilichapishwa na lilikusudiwa kuwashinda wapinzani wake wote. Kama matoleo ya awali ya Kiingereza – na matoleo ya enzi ile ile katika lugha zingine – hii ilitumia Maandishi ya Kiebrania ya Kimasorete na Maandishi Yanayopokewa ya Kigiriki (kutoka kwa familia ya Kibizantini). Watafsiri, waliosifika kwa haki kwa utauwa na usomi wao, walifanya kazi yao kwa uangalifu mkubwa. Kwa sababu hiyo, walitokeza tafsiri iliyo mwaminifu na sahihi zaidi, ambayo ingali isiyo na kifani katika mtindo wake wa fahari, usahili, na nguvu. Kwa kweli, toleo hili ndilo thamani ya asili ya toleo hili ambalo limeitwa "kitabu bora zaidi katika lugha yetu".

Matoleo ya kisasa yanakuja na yanakwenda, ambayo tunashukuru. Toleo hili hudumisha sifa yake, hata dhidi ya washindani makini kama Toleo Jipya la Mfalme Yakobo (The New King James Version).

Toleo Lililoidhinishwa, limethibitishwa kwa karne nyingi na kupendwa sana na watu wa Bwana, ni toleo bora kabisa na linasalia kuwa tafsiri bora zaidi ya Kiingereza ya Neno la Mungu lisilokosea na lisilo na makosa.

Malcolm Watts, mmoja wa maNaibu-Rais wa Trinitarian Bible Society, alizaliwa mwaka wa 1946 kule Barnstaple,North Devon, Uingereza. Alilelewa katika familia ya Kikristo, aliitwa kwa neema katika ujana wake na baadaye akaingia kwenye huduma ya kanisa. Alisoma pale Chuo kikuu ya Biblia ya London (London Bible College) mwaka wa 1967–70, na tangu 1971 amehudumu kama mchungaji wa Kanisa ya Emmanuel, mjini Salisbury. Yeye na Gillian walifunga ndoa mwaka wa 1976 na wamebarikiwa na watoto wawili wa kike, Lydia na Naomi.

Vidokezo

1 James Bannerman, *Inspiration: the Infallible Truth and Divine Authority of the Holy Scriptures* (Edinburgh: T & T Clark, 1865), p. 158.

2 Louis Gaussen, *Divine Inspiration of the Bible* (Grand Rapids: Kregel Publications, 1971. Published in Edinburgh in 1842 under the title, *Theopneustia: The Bible, its Divine Origin and Entire Inspiration, Deduced from Internal Evidence and the Testimonies of Nature, History, and Science*), p. 34.

3 This was the view of the older commentators, Piscator, Poole, Clarke, Gill, and others. More recently, it has been maintained by Dr. Greg L. Bahnsen in "The Inerrancy of the Autographa", a chapter included in the symposium entitled *Inerrancy*, edited by Dr. Norman L. Geisler (Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1980), p. 167.

4 William Henry Green, *General Introduction to the Old Testament: The Canon* (London: John Murray, 1899), p. 11.

5 Further information on the state of the text at this period may be found in John H. Skilton, "The Transmission of the Scriptures", in *The Infallible Word, a Symposium by the Members of the Faculty of Westminster Theological Seminary,* third revised printing (Philadelphia: Presbyterian and Reformed Publishing Company, 1967) pp. 153ff. See also Thomas Hartwell Horne, *An Introduction to the Critical Study and Knowledge of the Holy Scriptures*, seventh edition, (London: T. Cadell, 1834), 2:34.

6 Roger Nicole, "New Testament Use of the Old Testament", in *Revelation and the Bible*, Carl F.H. Henry, ed. (London: The Tyndale Press, 1959), pp. 142–43. See also the comments by Walter C. Kaiser Jnr, *The Uses of the Old Testament in the New* (Chicago: Moody Press, 1985), pp. 4ff.

7 Skilton, p. 143.

8 The Ante-Nicene Fathers, *Tertullian, On Prescription against Heretics*, chap. 36 (Grand Rapids: William Eerdmans Publishing Company, 1979), 3:260.

9 Dr A. Cleveland Coxe, who edited Tertullian's works for the original Edinburgh edition, concedes in a footnote that the "much disputed phrase ('their own authentic writings') may refer to the autographs or the Greek originals". However, he thinks that "probably" the reference is to "full unmutilated copies". Edward Miller (who edited several of Dean Burgon's works), appears to have believed that Tertullian was alluding to the original manuscripts. He wrote: "Tertullian, in arguing with heretics, bids them consult the autographs of the Apostles at Corinth, or Thessalonica, or Ephesus, or Rome, where they are preserved and read in public" *(A Guide to the Textual Criticism of the New Testament* [London: George Bell and Sons, 1886], p. 72).

10 The Ante-Nicene Fathers, *Polycarp, The Epistle of Polycarp to the Philippians*, chap. 12, 1:35.

11 J.P. Lilley, *The Pastoral Epistles* (Edinburgh: T & T Clark, 1901), p. 216.

12 Caspar Rene Gregory, *Canon and Text of the New Testament* (Edinburgh: T & T Clark, 1907), p. 309. Dr Gregory comments: "No one will imagine … that only those letters and not the book of Revelation were to be sent to the churches, for that verse (Revelation 1:11) says that John is to write in the book what he sees, that is to say the visions which follow, and send it to the churches" (p. 310).

13 The Ecclesiastical History and Martyrs of Palestine, *Eusebius, Ecclesiastical History,* book 3, chap. 37. (London: Society for Promoting Christian Knowledge, 1928).

14 Ibid., book 4, chap. 23.

15 Ibid., book 5, chap. 28.

16 Tertullian, chap. 38, 3:262.

17 The Ante-Nicene Fathers, *Irenaeus, Irenaeus against Heresies,* book 5, chap. 30, sect. 1, 1:558.

18 Kurt and Barbara Aland, *The Text of the New Testament: an Introduction to the Critical Editions and to the Theory and Practice of Modern Textual Criticism*, 2nd ed, 1989. Cited by Bruce M. Metzger in *The Text of the New Testament: Its Transmission, Corruption, and Restoration, third, enlarged edition* (Oxford: Oxford University Press, 1992), p. 262.

19 Benjamin B. Warfield, *An Introduction to the Textual Criticism of the New Testament* (London: Hodder and Stoughton, 1886), pp. 110, 111.

20 Harry A. Sturz, *The Byzantine Text-Type and New Testament Textual Criticism* (Nashville, TN: Thomas Nelson Publishers, 1984), pp. 61ff, 145ff.

21 Edward Miller in "The Antiquity of the Traditional Text", in John William Burgon, *The Traditional Text of the Holy Gospels Vindicated and Established* (London: George Bell and Sons, 1896), p. 121.

22 John Owen, "Of the Integrity and Purity of the Hebrew and Greek Text of the Scripture", in *The Works of John Owen* (London: The Banner of Truth Trust, 1968), 16:366.

23 B.H. Streeter, *The Four Gospels: A Study of Origins,* revised from the 1924 edition (London: Macmillan & Co. Ltd, 1956), pp. 112ff, 121ff.

24 F.H.A. Scrivener, *Six Lectures on the Text of the New Testament and the Ancient Manuscripts* (Cambridge: Deighton, Bell, and Co., 1875), pp. 41, 43.

25 Gordon H. Clark, *Logical Criticisms of Textual Criticism* (Jefferson, MD: The Trinity Foundation, 1986), p. 15.

26 B.F. Westcott and F.J.A. Hort, *Introduction to the New Testament in the Original Greek* (Massachusetts: Hendrickson Publishers, 1988. Originally published by Harper and Brothers, New York, 1882), p. 225.

27 Sturz, p. 84.

Malengo ya Jumuiya

- Kuchapisha na kusambaza Maandiko Matakatifu duniani kote katika lugha nyingi.

- Kuzikuza tafsiri za Biblia ambazo ni sahihi na za kutegemeka, zinazoambatana na Maandishi ya Kiebrania ya Kimasora la Agano la Kale, na Nakala iliyopokelewa ya Kiyunani la Agano Jipya, maandiko ambayo ndiyo msingi wa Toleo Lililoidhinishwa.

- Kuwa chombo katika kuleta nuru na uzima kupitia Injili ya Kristo kwa wale waliopotea katika dhambi na giza ya dini ya uongo na kutoamini.

- Kuyategemeza mafundisho ya Ukristo uliyorekebishwa, kuushuhudia uungu sawa na wa milele wa Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu, Mungu Mmoja katika Nafsi tatu.

- Kuitegemeza Biblia kama Neno la Mungu lililovuviwa, lisilo na kosa. Kwa Utukufu wa Mungu na kwa kuongezeka wa Ufalme Wake kupitia usambazaji wa matoleo ya Kiprotestanti yasiyopotoshwa ya Neno la Mungu.

Product Code: **SWHA111**

ISBN 978 1 86228 612 2

9 781862 286122

Trinitarian Bible Society

William Tyndale House, 29 Deer Park Road
London SW19 3NN, England

email: contact@tbsbibles.org
tbsbibles.org
tbsonlinebible.com